KUCHUNGUZA DHAMIRA NA FANI KATIKA NYIMBO BEMBELEZI ZA WATOTO: MIFANO KUTOKA MAKUNDUCHI

ZAINAB RAMADHAN HAJI

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2017

UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapo chini anathibitisha kuwa amesoma tasnifu hii iitwayo kuchunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto katika lahaja ya kimakunduchi na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digrii ya M.A Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

…….

Dkt. Mohammed Omary Maguo

(Msimamizi)

……..

Tarehe

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kumiliki kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa niaba.

TAMKO

Mimi **Zainab Ramadhan Haji,** ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika huo Kikuu chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyengine yoyote.

…….

Sahihi

…….

Tarehe

TABARUKU

Napenda kuitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu, mume wangu, ndugu zangu na watoto wangu.

SHUKURANI

Kazi hii ya utafiti ni matokeo ya mchango na ushirikiano mkubwa baina yangu na watu wengine, wakiwemo walimu wangu. Kwa kuwa sio rahisi kuandika mchango wa kila aliyenisaidia kuikamilisha kazi hii, wafuatao wanastahiki shukrani za kipekee. Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai, uzima, afya, nguvu na fahamu katika kipindi chote cha masomo yangu.

Pili, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa msimamizi wangu wa tasnifu hii, DKT. Mohammed Omary Maguo kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti huu. Hakusita wala hakuchoka kunishauri, kunielekeza na kuirekebisha kazi hii katika hatua zote mpaka ilipokamilika. Msaada wake hauwezi kukisiwa wala kulipwa. Ninachoweza kusema ni kutoa ahsante sana DKT. Omary Mwenyezi Mungu Akubariki na Akujaalie afya njema na maisha marefu. Aaamin, Aaamin, Aaamin.

Tatu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa walimu wengine wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa msaada mkubwa walionipatia katika kipindi chote cha masomo yangu. Walimu hao ni Sheikh, Profesa, Daktari, T.S.Y.M. Sengo, Profesa Emmanuel Mbogo, DKT. Anna Kishe, DKT. Hanna Simpasa, DKT. Zelda Elisifa, DKT. Hadija Jilala na DKT. Gress Kisasi.

Nne, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa familia yangu nikianzia na mume wangu mpenzi Amour Talib Ali, watoto wangu Luqman Amour Talib, Shayrin Amour Talib, Abutalib Amour Talib na Ajmaal Amour Talib, wazee wangu bi

Salama khamis Hassan na bwana Ramadhan Haji ambae ameshatungulia mbele ya haki nakuomba mwenyezi Mungu umpe maisha mema huko aliko.

Ninawashukuru sana kwa uvumilivu na mashirikiano muliyonipa katika kipindi chote cha masomo.

Pia ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wanafunzi wenzangu wapenzi kwa kuwa pamoja bega kwa bega katika hatua zote muhimu za utafiti huu kuanzia mwanzo mpaka kukamilika kwake.

IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia dhamira katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi. Ili kukamilisha lengo hili kuu, malengo mahsusi mawili yamepitiwa. Malengo hayo yalihusu kuchambua dhamira na mbinu za kisanaa zinazotumiwa na wasanii katika kusawiri dhamira zinazojitokeza ndani ya nyimbo za kubembelezea watoto mifano kutoka Makunduchi. Katika kukusanya data mtafiti alitumia mbinu ya kupitia machapisho, mbinu ya ushuhudiaji, mbinu ya kusikiliza na mbinu ya mahojiano pamoja na kutumia mbinu ya kimaelezo katika kuchambua data. Kwa ujumla utafiti umeweza kukusanya data ambazo zimeweza kujibu maswali ya utafiti huu. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kwamba, nyimbo bembelezi za watoto zina hazina kubwa katika kuonyesha dhamira ambazo zinakwenda sambamba na uhalisia katika maisha na jamii. Dhamira hizo ni kama mapenzi, nafasi ya mwanamke, ukweli, usaliti, siasa na uchumi. Pia, matokeo ya utafiti yanaonyesha kwamba mbinu za kisanaa zinazotumiwa na watunzi pamoja na wasanii katika uwasilishaji wa dhamira ni nyingi miongoni mwake ni kama taswira, ishara, sitiari, usimulizi, usambamba, nahau, tashbiha na takriri. Mwishoni mwa utafiti kumetolewa mapendekezo mbalimbali kwa ajili ya tafiti za baadaye kwa kupitia utanzu wa fasihi simulizi wa nyimbo kwa kuziangalia zaidi nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka sehemu nyengine zinazopatikana ndani ya nchi na katika lugha za makabila mengine nchini.

YALIYOMO

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Utafiti kuhusu nyimbo bembelezi umefanywa na wataalamu wengi wakiwemo (Finnegan, 1970 na Ali, 2013) kwa viwango mbalimbali lakini viwango hivyo havijafikia katika kiwango cha kutosheleza. Hivyo utafiti huu umekuwa kama ni chachu mojawapo ya kuchangia katika kuziba pengo, ili kukuza na kuimarisha tafiti katika nyimbo bembelezi katika fasihi ya Kiswahili. Sura hii ni sura tangulizi ambayo kwa ujumla wake inatoa mwongozo wa utafiti huu. Katika sura hii vipengele mbalimbali vimejadiliwa ili kuibua tatizo la utafiti huu. Vipengele vilivyojadiliwa ni usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, eneo la utafiti na mpangilio wa tasnifu.

1.2 Usuli Wa Mada

Fasihi simulizi ni fasihi inayotungwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya mdomo na vitendo bila ya kutumia maaandishi. Balisidya (1987) anafafanua kuwa Fasihi Simulizi ni aina ya fasihi ambayo hutumia mdomo na kuimbwa, kusambazwa kwa wasikilizaji na watumiaji wake. Fasihi simulizi ikiwa ni sanaa itumiayo maneno katika kutoa dhana fulani, hutegemea sana nyenzo mbalimbali za kuonekana na kusikika zitumiwazo na binaadamu kujieleza. Jambo la msingi ni kubaini fasihi simulizi katika uwasilishaji wake, ambapo katika kutolewa kwake fanani na hadhira wanakuwa pamoja, na huweza kusikilizana na kuelewana. Haji (1983) ameelezea fasihi simulizi kuwa ni chombo muhimu cha kuhifadhi

utamaduni wa jamii. Anaendelea kusema kuwa iwapo jamii inahitaji kuufufua utamaduni wake, haina budi kuvipa kipaumbele vipengele muhimu ikiwemo lugha. Kwa mujibu wa maelezo yake anaona kuwa, lugha ikiwa ni chombo na kielelezo kimojawapo cha jamii ni lazima iangaliwe kwa undani na mapana yake. Aidha, amesisitiza kuwa kuiangalia lugha kwa upande wa maandishi pekee si busara kwani kudhani kuwa kuimiliki sanaa ya uandishi ndio kigezo pekee cha ustaarabu, uhai na maendeleo ya jamii ni dhana potofu, kwani maandishi hayana historia kubwa katika maisha ya mwanadamu.

Njogu na wenzake (2001) wameonesha umuhimu mkubwa wa fasihi simulizi katika jamii ya Waswahili. Wakiainisha matumizi ya fasihi simulizi kuwa ni chombo cha kuwasilishia maadili ya jamii husika, pamoja na kuiburudisha, wanasema katika jamii zote fasihi simulizi imetumiwa kuwasilisha maadili na mafungu kemkem kuhusu jamii husika. Pia, imetumika ili kustarehesha na kuburudisha kwa namna inavyotumia lugha, uigizaji, utendaji, taharuki na mbinu mbalimbali za simulizi. Fasihi hujidhihirisha katika nyimbo na ngoma, mashairi, maigizo, ngano, methali, na vitendawili. Vile vile, nyenzo pekee yamawasiliano ya kijamii ni lugha; lugha isiyotumia sanaa huwa haiwasilishi ujumbe mzuri na kwa njia nzuri. Hivyo, fasihi simulizi ni njia nzuri ya kuwasilishia ujumbe kwa jamii na kwa namna iliyobora zaidi. Aidha, wanatoa maelekezo juu ya njia bora za ufundishaji wa lugha ya Kiswahili hasa upande wa fasihi simulizi na kuonesha namna hadithi, ushairi na tanzu nyengine za fasihi simulizi zinavyoweza kuwa chachu ya maendeleo ya jamii katika lugha. Pia, maelezo yao yametaja tanzu za fasihi simulizi kuwa ni nyimbo, ngoma, mashairi, maigizo, ngano, methali na vitendawili. Mulokozi (1989) ametaja tanzu za fasihi simulizi kama mazungumzo, masimulizi, maigizo, semi, ngomezi pamoja na ushairi. Utanzu wa mwanzo kabisa kuwepo hapa duniani ni ushairi tena ushairi simulizi tena ushairi wa nyimbo. Kwa kuwa kila moja ya tanzu hizi ni pana na ina mambo mengi ndani yake, ndio maana utafiti huu, ulijiegemeza katika utanzu mmoja peke yake, ambao ni utanzu wa ushairi na kugusia kipera cha nyimbo. Mulokozi(1996) anaendelea kusema kuwa fasihi simulizi ni tukio linalofungamana na muktadha fulani wa kijamii, na kutawaliwa na mwingiliano wa mambo sita kama vile fanani (msanii), hadhira, tukio, fani inayotendwa, mahali, na wakati. Mulokozi (ameshatajwa) hapo juu anasema kuwa tanzu za fasihi simulizi ni

nyingi, mfano mazungumzo masimulizi, maigizo, ushairi, semi na ngomezi ambazo hutofautiana kati ya jamii na jamii nyengine.

Haji (1992) anaieleza fasihi simulizi kuwa ni ile inayobuniwa bila ya kuandikwa. Akifafanua zaidi, anasema kuwa msanii huyatoa mawazo yake kwa kutumia maneno ya mdomo, yaani kwa kusimulia. Pia, amegusia juu ya chanzo cha fasihi simulizi kuwa ni uwezo wa binadamu wa kuwasiliana kwa maneno (lugha); na kuwa, kwa vile haifahamiki lugha ilianza lini, vile vile na fasihi nayo haifahamiki ilianza lini. Ameonesha pia kuwa fasihi simulizi ni yenye kurithiwa kutoka kizazi hadi kizazi. Akiainisha tanzu zake, amezitaja kuwa ni ngano, visasili, migani, tamthilia, vitendawili, methali na ushairi. Dhima za fasihi simulizi amezitaja za kuburudisha, kuidilisha, kuamsha na kudadisi. Hata hivyo, Mulokozi (1989) ametaja tanzu za fasihi simulizi kama mazungumzo, masimulizi, maigizo, semi, ngomezi pamoja na ushairi. Utanzu wa mwanzo kabisa kuwepo hapa duniani ni ushairi tena ushairi simulizi, na utanzu wa mwanzo kabisa kupata kuwepo hapa ulimwenguni ni ushairi wa nyimbo. Kwa kuwa kila moja ya tanzu hizi ni pana na ina mambo mengi ndani yake, ndio maana utafiti huu, ulijiegemeza katika utanzu mmoja peke yake, ambao ni utanzu wa ushairi na kugusia kipera cha nyimbo.

Ndungo, na Wafula (1993) Wanasema, kuna nyimbo ambazo huimbwa kuwabembeleza watoto katika makabila mbali mbali. Nyimbo hizo huwa na utaratibu maalumu. Waswahili pamoja na makabila mbali mbali ya kiafrika huwa na desturi ya kuwaimbia watoto wao wachanga au wadogo nyimbo nzuri ili wapate kulala, kusimulia yaliyomo ndani ya nyoyo zao au kuwanyamaza wakiwa wanalia. Nyimbo hizo za kubembeleza watoto huimbwa kwa sauti nzuri zenye mahadhi mazuri yenye kupendeza masikioni mwa watoto hao wachanga au wadogo. King'ei (1997) anasema, kuna nyimbo za furaha na pia kuna nyimbo za huzuni inategemea na tukio au sherehe husika. Fani iitwayo nyimbo ni moja wapo ya tanzu maarufu katika fasihi simulizi kwa tamaduni zote. Ni ukweli usiopingika kuwa uzuri wa nyimbo huonekana zaidi pale muimbaji anapoonyesha utaalamu wake katika kughani na kupangilia vizuri maneno yake. Jambo hili humsaidia sana muimbaji kuteka mawazo na fikra za hadhira yake na kuifanya iwe makini katika usikilizaji wake, hali hii husaidia kufikia ujumbe uliokusudiwa kwa urahisi na pia jamii hufunzika kutokana na ujumbe huo. Aidha jamii zinatofautiana kiutamaduni katika mila, desturi na silka za watu kutokana na maeneo wanayotokea. Hivyo basi, nyimbo nazo huwa tofauti kulingana na matukio au matendo yaliokusudiwa na nyimbo husika. Katika fasihi ya Kiswahili, utanzu wa ushairi na nyimbo umeingiliana na kuathiriana sana kimuundo na kimtindo.

Karisa (2000) anasema fasili ya nyimbo ni maneno yaliopangwa na kupewa mahadhi fulani kwa madhumuni ya kuimbwa. Mahadhi (mdundo) yanatakikana yalingane na midundo ya maneno yaliomo katika wimbo. Aidha ni lazima ala za muziki ziambatane na wimbo na mdundo wake. Wimbo ni lazima uwe unaweza kumfanya mtu atingishe kichwa ama apige chini wayo wake akifuata mdundo au mahadhi ya wimbo. Nyimbo zilitungwa juu ya mapenzi, kusifu na kutia ila, zilikuweko pia nyimbo za kufungia wanyama. Miongoni mwa nyimbo alizozielezea Karisa ni nyimbo bembelezi ambapo amesema kuwa ni nyimbo za kuongoa watoto kwa madhumuni ya kuwabembeleza watoto ili walale au waache kulia, na ndizo ambazo tumeshughulika nazo katika utafiti kwa kuchunguza dhamira za nyimbo hizo.

Othman (2007) anasema nyimbo bembelezi ni za tangu zamani kwani wazee huwabeba watoto wao migongoni au huwapakata na kubembea ili wanyamaze kulia. Nyimbo hizi huwa na sauti ya polepole ya taratibu na ya kusihi, huwa fupi fupi hurudiwa rudia hadi mtoto alale au anyamaze kulia. Katika nyimbo hizi miongoni mwa mambo mengine mengi, wazee huwaombea dua watoto wao wakue kwa haraka na pia huelezea mahitaji muhimu ya mtoto ambayo ni chakula, elimu na malazi.

M’ngaruthi (2008) anasema uteuzi na mpangilio wa maneno maalum katika mashairi na nyimbo huibua hisia zinazohusiana na tukio. Hisia hizi ni kama vile furaha huzuni, uchungu, hasira, utulivu wa moyoni, chuki au hata mwamko fulani. Kwa ujumla ushairi una nguvu na mvuto wa ajabu. Anaendelea kusema na bembelezi ni miongoni mwa kipera cha fasihi simulizi. Neno bembelezi linatokana na kitenzi bembeleza chenye maana ya tuliza au nyamazisha mtoto anayelia (ongoa) (TUKI 2004 NA BAKIZA 2010).

Mulokozi (1996) anasema nyimbo ni kile kinachoimbwa. Anaendelea kusema nyimbo ni dhana pana inayojumuisha tanzu nyingi, baadhi ya tanzu za kinathari zinazoingia katika utanzu huu ni kama vile hadithi huweza kuingia katika kundi la nyimbo pindi zinapoimbwa. Mambo yanayotambulisha nyimbo ni kama vile muziki wa sauti ya muimbaji au waimbaji, muziki wa ala, matini au maneno yanayoimbwa, hadhira inayoimbiwa na muktadha unaofungamana na wimbo huo, mfano sherehe, ibada, kilio, kubembelezea watoto (bembea au pembejezi) n.k. Hivyo basi, nyimbo bembelezi ni miongoni mwa kipera cha fasihi simulizi, Mulokozi (ameshatajwa) anasema bembea ni nyimbo za kubembelezea watoto. Nyimbo hizi ziko nyingi sana kwa kutegemea na kila kabila na huibua maudhui mazito kwa jamii. Wataalamu na watafiti mbali mbali wamezungumzia mambo mengi kuhusiana na nyimbo.

Hivyo basi, waswahili wa kusini Makunduchi Zanzibar nao hutumia nyimbo bembelezi katika kuwabembeleza watoto wao, kwa sababu hiyo; mtafiti ameona ipo haja ya kuchunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi. Kwani kunaonekana kuwa siku hizi kutokana na sayansi na teknolojia na utandawazi ulioenea wazazi au walezi wengi hawatumii nyimbo hizo isipokuwa hutumia simu na komputa zenye vibonzo ndani yake kwa kufunguliwa simu hizo au komputa na kuwekewa watoto wakiwa wanaangalia au kuchezea na huacha kulia. Baadhi ya wazazi hutumia bembea zenye kengele ndani yake ambazo hubonyezwa kengele hizo pale mtoto anapolia ili anyamaze. Pia kuna utatanishi na kumpelekea mtafiti kujiuliza masuali mbalimbali kama; Jee nyimbo hizo huimbwa kunyamazisha watoto au kuna jambo jengine ndani yake? Mawazo ya wataalamu hawa kwa pamoja imekuwa ni chachu iliyompelekea mtafiti kuangalia kwa kina nyimbo bembelezi na kufanya utafiti utakao husisha uchunguzi wa dhamira za nyimbo bembelezi.

1.3 1.2 Tatizo la Utafiti

Kumekuwa na malalamiko kwamba vipera vya fasihi simulizi havijafanyiwa tafiti za kutosha kama ilivyobainishwa na Mazrui na Syambo (1992), Masebo na Nyangwine (2004) na hili limejitokeza katika nyimbo bembelezi. Imeonekana kuwa tafiti kadhaa zimefanywa katika fasihi, Kazi nyingi za kihakiki hushughulikia fasihi kwa ujumla hususan fasihi andishi kama vile tamthilia na riwaya lakini mtafiti aligundua tafiti chache zilizofanywa katika kipera cha nyimbo bembelezi za watoto, aidha hakuna tafiti za kina ziliyofanywa juu ya nyimbo bembelezi za watoto katika eneo tajwa.

Mtafiti anaona kwamba nyimbo bembelezi za watoto ambazo zinazungumzia mambo yote yanayohusu jamii kama ukweli, mapenzi, malezi na mambo mengineyo

zinapotea kwa kasi na wazee ambao wanazijua nyimbo hizo wamekuwa wakirudi kwa Muumba kila kunapokucha. Mtafiti ameona ipo haja kubwa ya kufanya utafiti wa nyimbo za watoto katika eneo lililoteuliwa kwa kuzihuisha na kuzihifadhi ili ziweze kutumika katika jamii ya sasa na ijayo. Tatizo kuu la kupotea na kusahaulika kwa nyimbo hizo kunasababishwa na utandawazi wa kutumia bembea zenye kengele, simu za mkononi na runinga zenye katuni ambapo hupelekea kutotumika kwa nyimbo hizo.

Hivyo basi utafiti huu umefanywa ili kuziba pengo hilo la kiutafiti kwa kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi.

1.4 1.3 Malengo Ya Utafiti

1.3.1 Lengo Kuu La Utafiti

Kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi.

1.3.2 Malengo Mahsusi

(i) Kuchambua dhamira zinazopatikana ndani ya nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi.

(ii) Kubainisha mbinu za kisanaa zilizotumiwa na wasanii katika kusawiri dhamira zilizopatikana katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi.

1.5 1.4 Maswali Ya Utafiti

Utafiti huu umelenga kujibu maswali yafuatayo:

(i) Ni dhamira zipi zinazopatikana ndani ya nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi.

(ii) Ni mbinu zipi za kisanaa zinazotumiwa na wasanii katika kusawiri dhamira za nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi.

1.6 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa muhimu kwa taaluma hasa katika fasihi simulizi. Katika fasihi simulizi utafiti huu utakuwa na umuhimu katika kuutajirisha utanzu wa ushairi – simulizi. Aidha, utafiti huu utasaidia kupata uhai mzuri wa fasihi simulizi ya waswahili ambayo kwa kiasi kikubwa umeathiriwa kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia duniani, kama anavyosema Ali (1969) “ nyimbo hizi ni za zamani zilikuwa zikitumika sana hapa petu unguja na pwani ya Afrika ya mashariki. Siku hizi hazisikilikani tena majumbani, zimeanza kupotea na kusahaulika kidogo kidogo na mpaka mwisho baada ya muda si mrefu zitapotea kabisa”.

Kwa upande wa utamaduni, utafiti huu utatoa mchango mkubwa katika kuelewa mchango wa utamaduni wa Makunduchi hasa kipengele cha lugha katika maendeleo ya nyimbo za watoto, pia utafiti huu utasaidia uimarishaji wa silka, mila na utamaduni wa jamii katika maisha yao ya kila siku. Vile vile utatoa mchango mkubwa wa kupata maarifa ya makuzi na malezi yanayosaidiwa na nyimbo za kubembeleza watoto kwa vijana wa Makunduchi na sehemu yote ya Unguja. Kwani utasaidia katika kuhifadhi nyimbo za Makunduchi kwa ajili ya kizazi hadi kizazi.

Pia utafiti huu ni chachu ya kuleta mwamko kwa watafiti wa fasihi simulizi hasa katika nyanja ya nyimbo za watoto za jamii mbalimbali. Watafiti wanapaswa kujitoa kwa moyo, kusoma kwa mzamo nyanja hii ya nyimbo za watoto na kuandika makala zitakazosaidia kuhifadhi hazina hii adhimu, ambayo kwa sasa ipo hatarini kupotea,

na kwa sasa jamii inatakiwa kutumia hadhina hii katika malezi ya watoto na kurekebisha maadili yanayokengeuka kila uchao.

Kwa upande wa kisiasa utafiti huu utakuwa muhimu upande huo, kwani wanajamiii wanaweza kubaini kwamba nyimbo bembelezi si muhimu katika katika sekta ya kielimu, kijamii na kiutamaduni tu, bali pia ni muhimu hata katika mambo ya kisiasa kwani nyimbo hizo zinaweza kutoa maudhui ya kisiasa kutegemea na nyimbo na uchambuzi wa mtafiti.

Hivyo, utafiti huu utakamilisha kuziba pengo kuhusu dhamira ya nyimbo bembelezi za watoto katika jamii ambayo ilikuwa haijafanyiwa utafiti wa kutosha. Mwisho utafiti huu utakuwa rejeleo muhimu katika ushairi simulizi wa Kiswahili kwa waalimu, wanafunzi, wadau wa fasihi na watafiti wengine wa baadae ambao watakuja shughulikia vipengele ambavyo havijaangaliwa kwa undani kijumla.

1.7 1.6 Mipaka ya utafiti

Utafiti huu umefanyika Zanzibar, Kisiwa cha Unguja, Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Kusini, katika cha Makunduchi. Ni eneo la kijiografia la utafiti huu. Utafiti huu umeshughulikia kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto:mifano kutoka Makunduchi ambapo mtafiti amehusisha mitaa minne tu ya kijiji hicho nayo ni Kiongoni, Kumbini, Mtaandani na Kajengwa.

Kwa upande wa mipaka ya kinadharia, utafiti huu umehusisha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na nadharia ya Semiotiki.

1.8 1.7 Mpangilio Wa Tasnifu

Tasnifu hiii imekuwa na jumla ya sura tano zenye mada kuu na mada ndogo ndogo ndani yake. Sura ya kwanza imeelezea vipengele mbalimbali vya kiutangulizi, vipengele hivyo ni usuli wa mada, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, malengo mahsusi ya utafiti. Maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasnifu. Sura ya pili imehusisha mapitio ya kazi tangulizi, pamoja na nadharia teule zilizotumika katika utafiti huu. Sura ya tatu imeelezea mbinu za utafiti, katika sura hii imehusisha mbinu za ukusanyaji wa data, mbinu za usampulishaji na aina za data zilizokusanywa pamoja na kuonesha mbinu za uchambuzi wa data za utafiti huu. Sura ya nne imehusisha uchambuzi wa data za utafiti uwasilishwaji na kujadiliwa. Sura ya tano ni ya mwisho ambayo imetoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti wa baadae.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA YA KINADHARIA

2.0 Utangulizi

Kazi tangulizi zina umuhimu mkubwa kwa watafiti kwani zinamuelekeza mtafiti au mchunguzi wa jambo kupekuwa taaluma iliyofichwa na kujua pengo liliopo kwenye utafiti wake au kwenye kazi yake, katika kulitekeleza hili mtafiti au mchunguzi wa jambo hana budi kusoma vitabu, majarida, magazeti, kupitia mitandao na kazi zilizotangulia. Omar (2011) anasema kuwa kazi tangulizi hutoa ujuzi na maarifa ya wanazuoni waliowahi kufanya kazi yenye muelekeo na lengo la mtafiti wa utafiti huu. Katika sura hii mtafiti amegawa utafiti katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza imehusu mapitio ya kazi tangulizi na sehemu ya pili imezungumzia kiunzi cha nadharia.

2.1 Ufafanuzi wa Istilahi

Katika tasnifu hii zimetumika istilahi, istilahi hizo ni muhimu kwa msomaji na msikilizaji wa nyimbo bembelezi. Kwa hivyo, sehemu hii inatoa orodha ya istilahi hizo na maana yake kwa lengo la kumsaidia msomaji aelewe kwa urahisi.

2.1.1 Bembelezi

Finnegan (1970) anasema bembelezi ni nyimbo ambazo mama au mlezi humuimbia mtoto wake, ni nyimbo za watoto lakini huimbwa na watu wazima kwa sababu wao ndio wenye jukumu na wajibu wa kuwalea watoto. Kwa maana hiyo, mama au mlezi huwasilisha hisia zake, mawazo na matarajio yake kutokana na kuathiriwa na baadhi ya mifumo.

Karisa (2000) anasema bembelezi ni nyimbo za kuongoa watoto kwa madhumuni ya kuwabembeleza walale ama waache kulia. Karisa anaendelea kusema kuwa, lengo kuu la nyimbo bembelezi ni kutoa hisia kwa yule mbembelezaji ambae ametokezewa na misukosuko, hivyo huamua kutoa nyimbo ili kufikisha lengo lake kwa wahusika. Wamitila (2003) anasema bembelezi hukusudiwa kumlaza mtoto au kumuongoa aache kulia, huweza pia kutumiwa kupitisha ujumbe fulani. Wamitila anaendelea kusema kuwa bembelezi huweza kutumiwa kama njia ya kumpiga vijembe mzazi wake ikiwa anaehusika ni mlezi. Hivyo basi, kwa mujibu wa wataalamu hawa nyimbo bembelezi zina madhumuni maalum mbali na kuwa huwabembeleza zaidi watoto kuacha kulia. Hivyo katika nyimbo hizi mumeibuka dhamira mbalimbali ambazo zimewasilishwa na wasanii katika jamii.

2.1.2 Dhamira

Dhamira ni lengo au shabaha ya kazi ya fasihi (Njogu na Chimerah, 1999). Kwa mujibu wa Kamusi la Kiswahili fasaha Bakiza (2010) dhamira ni jambo linalozungumzwa katika kazi ya fasihi. Senkoro (2011) anaeleza kuwa katika dhamira kuu tunaweza kugundua dhamira ndogo ndogo zinazoambatana na dhamira kuu. Hivyo dhamira ni wazo kuu linalotawala kazi ya kifasihi kuanzia mwanzo mpaka mwisho, wazo hili hukuzwa kwa njia zilizo wazi. Aidha dhamira ni lengo, kusudio, ujumbe, idadi, au wazo ambalo hupatikana katika kazi ya fasihi kupitia uhakiki au uchambuzi wa kazi hiyo.

2.2.1 Kazi Tangulizi Zinazohusu Nyimbo kwa Ujumla

Katibula (1975) anasema nyimbo ni aina ya fasihi simulizi yenye namna pekee ya kujieleza, kila mtu huweza kuitumia bila ubaguzi kwa wakati wowote anapojisikia. Anasisitiza kuwa nyimbo ni chombo cha kujifurahisha, kuonesha huzuni, kutoa mashambulizi na kuhami. Mawazo haya ya Katibula mtafiti anakubaliana nayo na yameweza kumsaidia kuchunguza nyimbo za kubembelezea watoto ili aweze kubaini ni kwa vipi nyimbo hizo zinatumika kwa namna ya upekee katika kujieleza na kutoa dhamira mbalimbali kwa jamii.

Nkwera (1978) anasema nyimbo huwa ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki. Anafafanua maana ya muziki kwa kusema ni mpangilio wa sauti za ala na uimbaji unaoleta athari fulani kwa binadamu kupitia hisi zake na pia akili yake. Nkwera ameshatajwa anamalizia kwa kusema kuwa kilicho muhimu ni maneno ya uimbaji na sauti za ala, miondoko sio lazima. Maana ya nyimbo iliyotolewa na Nkwera mtafiti anakubaliana nayo kuwa ni maneno ya uimbaji jambo ambalo limempelekea mtafiti kuweza kuchunguza nyimbo bembelezi za watoto.

Mbarouk (1983) aliandika juu ya nyimbo za michezo ya watoto kisiwani Pemba na kusema kuwa kila jamii ya watu huwa na michezo yake ya jadi ambayo huchezwa na watoto wa jamii ile. Anaendelea kusema kuwa michezo hii mara nyingi huambatana na nyimbo. Katika kisiwa cha Pemba iko michezo mingi ya watoto nayo hutofautiana kila mtaa au pahala huwa na aina yake ya michezo ingawa mara nyengine michezo fulani inaweza ikaonekana kila mahali. Mbarouk (ameshatajwa) anaendelea kusema kuwa zikichunguzwa nyimbo zinazoimbwa katika michezo hii, nyingi zinaonekana hazina maana kamili, lakini huimbwa ili zilingane na mshindo na mpangilio wa michezo. Anamalizia kwa kusema kuwa ziko baadhi ya nyimbo

ambazo zina maana kamili na kuwa zinatoa mafunzo fulani. Kinyume na makala ya Mbarouk ambae amezungumzia nyimbo za michezo ya watoto kuwa ni aina nyingi, mtafiti wa utafiti huu amechunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi.

Mazigawa (1991) amefasili wimbo kuwa ni kifungu cha maneno yaliopangwa katika utaratibu maalumu wenye kutekeleza mapigo ya muziki. Aghalabu lugha yake huwa ni ya mkato ambayo hufuata mapigo ya ala ya muziki kwa mfano ngoma, zeze, marimba, njuga, filimbi n.k. nyimbo pia huenda sambamba na ngoma kwani wakati wa kuuimba ngoma huendelea kulia na wakati huo huo waimbaji hucheza. Pia, wengine huimba kwanza halafu ngoma hufuatia na wachezaji hufuata mlio wa ngoma. Nyimbo bembelezi kwa kawaida hazifuati mapigo ya ngoma wala midundo, lakini waimbaji wake huzipanga katika mtiririko wenye kufuata vina na mizani na kuleta mantiki iliyokusudiwa kwa wahusika.

Haji na wenzake (1992) wamefasili kuwa nyimbo ni mashairi mafupi hujitokeza katika sehemu nyingi za jamii. Wameendelea kwa kusema nyimbo huwa ni fupi aghalabu huwa ni ubeti mmoja tu wenye mistari mitatu. Nyimbo huweza kuambatana na sanaa ya kughani, ngoma, makofi au muziki. Watafiti hawa wametuonyesha kuwa nyimbo zaweza kuwa na ubeti mmoja au zaidi jambo ambalo limempelekea mtafiti kuweza kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto, nyimbo ambazo kwa kawaida huwa na beti moja au mbili.

Njogu na Chimerah (1999) wameeleza kuwa nyimbo zinatokana na ushairi ambao ndio utanzu wa fasihi ulio mkongwe. Ambazo zilianzia na hisia za matukio yaliyowakuta watu katika miktadha na mandhari ya maisha yao ya raha na furaha, ugumu, kujituma, ama machungu na ushujaa. Anafafanua kwa kusema kwamba

katika jamii za kilimwengu. Wimbo ulianza wakati binadamu alipobuni lugha, jambo ambalo lilimtoa mtu katika hali ya uhayawani na kumfanya kiumbe razini. Mabadiliko haya yalimfanya mtu ayaelewe mazingira yake na aweze kutoa mchango wake katika kuyakabili na kuyabadilisha mazingira hayo. Mawazo ya wataalamu hawa yamemuwezesha mtafiti kuyatumia na kuuendeleza utafiti huu, ili kuweza kuchunguza dhamira za nyimbo za kubembelezea watoto.

Wamitila (2003) anasema kuwa tungo za utanzu wa nyimbo zina mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Tungo hizi huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha, na mapigo ya silabi ambayo hupangwa kwa utaratibu au muwala wenye mapigo ya kimuziki au wizani. Ingawa kanuni ya ala si ya lazima katika kuainisha nyimbo, inawezekana wimbo ukaambatana na ala, kwa mfano chapuo, vugo, ngoma, marimba, pembe na zumari. Wamitila (ameshatajwa) ameelezea nyimbo kuwa lugha yake ya mkato na matumizi ya picha, mitindo hii vile vile inapatikana katika nyimbo za kubembelezea watoto hata kama nyimbo hizi hazina mapigo ya ala.

King'ei na Kisovi (2005) pia wamefasili nyimbo kuwa ni utungo wenye mpangilio maalum wa maneno na una mahadhi. Wamesema nyimbo huambatana na shughuli au jambo fulani, na sauti ya mwimbaji au waimbaji huwatia moyo watu kama vile wavuvi au wakulima katika kazi zao. Vile vile, nyimbo huimbwa kwa burudani katika sherehe kama vile harusi, ibada za kidini, kafara, matambiko na katika tohara za jando au unyago. King'ei na Kisovi wamesema nyimbo huambatana na shughuli au jambo fulani, mawazo ambayo yamempelekea mtafiti kuweza kuchunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto kwani nyimbo hizi hutokezea katika muktadha maalum.

Thabit (2007) ameeandika tasnifu yake juu ya nafasi ya maudhui ya nyimbo za taarab katika jamii ya Zanzibar ya leo. Katika maandiko yake amesema kuwa nyimbo za taarab zinatoa maadili makubwa sana katika jamii husika lakini hakuishia hapo amependekeza nyimbo nyengine zifanyiwe kazi katika vipengele vyengine ambavyo bado havijafanyiwa kazi. Utafiti wa Thabit umekuwa chachu ya kumpelekea mtafiti kuchunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto.

Hamadi (2008) anasema, nyimbo ni sanaa ya lugha ya maneno yanayoeleza hisia na fikra, huwa teule, yalio finyangwa finyangwa na kusukwa kwa nidhamu na mvuto unaopendezesha muimbaji na kumvutia msikilizaji. Mtafiti huyu ameeleza kuwa nyimbo hutoa hisia na fikra kwa maneno teule kwa msikilizaji jambo ambalo limempekea mtafiti kuchunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto kwani katika nyimbo hizi mara nyingi waimbaji hutoa hisia zao kwa jamii.

Gora (2011) amefanya utafiti juu ya mitindo ya nyimbo za uganga wa pepo, katika utafiti huu amegundua kwamba kuna msamiati wa kiganga unaotumika katika nyimbo za uganga. Utafiti huu umechunguza na kuchambua mitindo ya nyimbo za uganga wa pepo katika kufanya hivyo, kilichojitokeza ni kuwa utafiti uligundua kuwa nyimbo za uganga wa pepo katika kisiwa cha Kaskazini Unguja zina misamiati yake. Gora ameonesha na kugundua misamiati mbalimbali katika nyimbo za uganga wa pepo pamoja na mitindo inayotumiwa na waganga hao katika nyimbo za pepo. Kinyume na Gora utafiti huu umelenga kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi.

Mzee (2011) katika makala yake isemayo “Athari za nyimbo za mipasho kwa jamii ya Wazanzibari” anasema kuwa nyimbo za mipasho ni maarufu sana hivi sasa. Nyimbo hizi, licha ya kufanana na zile za taarabu asilia pia zinatofautiana sana.

Tofauti hiyo huletwa na matumizi ya lugha isiyo na uficho, lugha kali yenye tashtiti na masimango ndipo jina hili la mipasho likatumika zaidi na si kwa maana ya kisarufi ambayo ni kutoa taarifa au habari. Hivyo Mzee (ameshatajwa) amesaidia sana katika kujua nyimbo zinazoimbwa katika taarab, kinyume na utafiti wa Mzee utafiti huu umelenga kuchunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto kwani katika nyimbo hizi watumiaji wake hutumia lugha ya mficho katika kuwasilisha dhamira na hisia zao.

2.2.2 Dhamira za Nyimbo kwa Jumla

Msokile (1981) amesema kuwa dhamira za nyimbo ni muhimu zilingane na hadithi kwa maana ya kuwa ujumbe unaopelekwa kwa jamii ukubaliane na jamii yenyewe. Kwa hivyo, dhima ya msanii ni kupima hadhira yake na kuisanifu nyimbo yake kulingana na hadhira aliyoikusudia. Pamoja na kuzingatia mabadiliko ya jamii anayoilenga. Msokile ameeleza kuwa dhamira za nyimbo ni muhimu zilingane na hadithi, mtaalamu huyu ametilia maanani zaidi kulingana kwa dhamira za nyimbo na hadithi, hakujishughulisha na nyimbo bembelezi za watoto ambapo mawazo yake ni chachu na yametoa mchango mkubwa kwa mtafiti kutokana na kutufahamisha dhima kuu ya msanii ni kupima hadhira na kuusanifu wimbo kulingana hadhira aliyokusudia. Kwa hivyo, mtafiti wa utafiti huu ametilia mkazo zaidi katika kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto.

Mulokozi (1989) ameeleza kwamba nyimbo zina dhima ya kuburudisha, kuelimisha, kuonya na kutia hamasa vitani. Anasema kwamba wasanii wa nyimbo wanapotunga na kuimba nyimbo zao mara zote wanakwenda sambamba na mambo ya kijamii yanayohusu nyanja mbalimbali ikiwemo siasa, uchumi na utamaduni kwa jamii. Ili

watoe ujumbe kulingana na muktadha wake juu ya tukio au jambo linalohusika. Anaendelea kusema nyimbo zinazotungwa katika jamii zinalenga katika kutekeleza majukumu kadhaa, kama vile kusifu mafanikio, kuwakosoa watu wazembe katika jamii, kujifurahisha, kupunguza uchovu, na kurithisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Maelezo ya mtaalamu huyu yamemsaidia mtafiti na kutoa mchango mkubwa katika utafiti wake kwa kuweza kubainisha na kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi.

Sengo (1995) amesema kuwa, katika unyago na jando la waswahili, wari huimbiwa nyimbo kama ni sehemu ya dawa na kuombewa wapone haraka. Anasema hivi, “Katika unyago na jando hufanyiwa uganga wari huimbiwa nyimbo kama dawa, ingawa hakueleza kingine chochote kuhusu nyimbo za uganga wa pepo isipokuwa ametaja tu aina za uganga kwa jumla. Maelezo ya mtaalamu huyu yamegusia ukweli wa mambo kwamba unyago na jando la waswahili, wari huimbiwa kwa lengo la kuwawezesha wapone haraka, na pia huimbiwa nyimbo ikiwa ni kama dawa ambapo hupata kujifunza kupitia unyago na jando hilo. Pamoja na kuwa alizungumzia juu ya lengo la nyimbo za jando na unyago katika jamii ya waswahili, ufafanuzi wake umetoa mchango muhimu wa kufanikisha lengo la utafiti huu kwani yeye hakugusia dhamira za nyimbo bembelezi, maelezo yake yalitumika kama dira ya kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto.

Mulokozi (1996) amefafanua kwamba, nyimbo zina kazi ya kuburudisha watu kwenye sherehe, au wakati wa mapumziko. Pia nyimbo hutumika kwa kufunza, kuarifu, kunogesha hadithi, kuomboleza, kubembeleza mtoto ili alale, hutumika katika kuchapuza na kutia hamasa vitani. Mtaalamu huyo ametilia maanani zaidi katika kuburudisha kwenye sherehe na mapumziko, kufunza na pia kubembeleza ili

mtoto alale, hakujishughulisha na dhamira zilizomo kwenye nyimbo hizo. Kwa hivyo, mtafiti wa utafiti huu ametilia mkazo zaidi katika kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto kipengele ambacho kinaonekana kusahaulika.

2.2.3 Kazi Tangulizi Kuhusu Nyimbo Bembelezi

Finnegan (1970) alizungumzia nyimbo na michezo ya watoto katika jamii mbalimbali barani Afrika. Alizikusanya na kuziainisha nyimbo na michezo waliyoimbiwa watoto wa shule za chekechea na zile za msingi. Aidha amefafanua uamilifu wa nyimbo husika, kwa mfano anaeleza nyimbo bembelezi kwa jamii ya Wabonyoro, nyimbo hizo zikiwa na dhima ya kubembeleza mtoto ili anyamaze kulia. Nyimbo za aina hii zilitumiwa na Mayaya ili kuwasilisha hisia zao kuhusu dhulma walizotendewa na matajiri wao. Finnegan alieleza madhumuni na kuonyesha umuhimu wa nyimbo hizi kwa jamii za kiafrika. Ambapo mtafiti wa utafiti huu amechunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto kwani mawazo ya mtaalamu huyu yamempa muongozo mtafiti wa utafiti huu.

Haji na wenzake (1992) wamefasili nyimbo za kuchombezea watoto kuwa ni nyimbo ambazo huimbiwa mtoto mchanga kwa ajili ya kumburudisha. Kwa kawaida huimbwa kwa ajili ya kumbembeleza mtoto wakati mama anapofanya kazi zake za nyumbani na huenda mtoto huyo amembeba mgongoni au amemlaza karibu nae. Mawazo ya wataalamu hawa yamekuwa chachu na yameakisi katika kuupeleka mbele utafiti huu.

Akivaga na Odaga (1992) wameeleza mengi kuhusiana na nyimbo. Hata hivyo maelezo yao yamelenga katika nyimbo za watoto. Wanaeleza kuwa nyimbo za watoto ni zile zinazoimbwa na wazee hasa wazazi na jamaa kumsifu mtoto na

aghlabu huimbwa na Mayaya kwa kusudi la kuwabembeleza watoto. Aidha wanaendeleza kueleza kuwa nyimbo bembelezi hizi huimbwa kwa utaratibu na kwa sauti nyororo, uamilifu wa bembelezi wanavyodai ni kudokeza au kubainisha jambo fulani kuhusu jamii husika. Pia wanadai kuwa nyimbo za watoto ziliimbwa kwa lengo la kuwaelimisha watoto tangu wakiwa wachanga juu ya amali za jamii na kile ambacho jamii ilitarajia kutoka kwao katika utu uzima wao madhumuni ni kuweza kutumia nyimbo katika kushajihisha maadili mema kwa watoto. Kwa hivyo mawazo hayo kwa kiasi yamemsaidia mtafiti katika kuchunguza dhamira na katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi.

Kapury (1993) alitafiti nyimbo za watoto miongoni mwa wamasai na ametoa mfano mmoja wa nyimbo bembelezi. Muktadha wa nyimbo hizi huwa ni nyumbani wakati mama hayupo. Wimbo huu huimbwa na msichana akimuimbia mtoto mdogo. Ingawa wimbo huu hudhihirisha sifa za kishairi, mtaalamu huyu hakuhakiki dhamira za nyimbo bembelezi alihakiki nyimbo za watoto wa jamii ya kimasai. Kapury amefanya utafiti katika kabila la kimasai kinyume na utafiti wa Kapury utafiti huu umeangalia upande mwengine wa kijamii kwa kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi.

Ndungo na Wafula (1993) wanasema kuna nyimbo ambazo huimbwa kuwaongelea watoto katika makabila mbalimbali. Nyimbo hizo huwa na utaratibu maalumu. Waswahili pamoja na makabila mbalimbali ya kiafrika huwa na desturi ya kuwaimbia watoto wao wachanga au watoto wao wadogo nyimbo nzuri ili wapate kulala au wapate kunyamaza wakati wakilia. Nyimbo hizo huimbwa kwa sauti nzuri na mahadhi mazuri yenye kupendeza masikioni mwa watoto wachanga hao. Ndungo na Wafula wameeleza uzuri wa sauti na mahadhi mazuri juu ya nyimbo hizo za

kubembelezea watoto katika makabila mbalimbali ya kiafrika. Kinyume na mawazo ya wataalamu hawa utafiti huu umechunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto katika kijiji cha Makunduchi, kwani mawazo ya wataalamu hawa yamekuwa chachu katika kuusaidia utafiti huu.

Naye Mulokozi (1996) amesema bembea ni nyimbo za kubembelezea watoto. Nyimbo hizo huweza kuwa na maudhui mazito na mengi yao aghalabu humhusu mwanamke na hali yake katika jamii na uhusiano wake na mama. Mulokozi ameelezea umuhimu wa nyimbo za kubembelezea watoto na dhamira zake kuwa ni nzito jambo ambalo limempelekea mtafiti kupata hamasa ya kuchunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto.

Pia Andanenga (2002) katika kufafanua nyimbo za watoto anasema nyimbo nyingi za namna hii zinaimbwa kwa ajili ya watoto, yaani akina mama na akina dada wanawaimbia watoto wadogo ili kuwabembeleza, kuwatuliza, kuwatumbuiza wapate kulala. Andanenga amefafanua nyimbo nyingi zinazoimbwa kwa ajili ya watoto wadogo mchango ambao umemfanya mtafiti aweze kuchunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto, kwa vile maelezo ya mtaalamu huyu yaliakisi zaidi kwa mifano ya nyimbo tofauti zinazotumiwa kwa ajili ya watoto.

Senkoro (2005) anasema kuwa nyimbo hizi aliimbiwa mtoto na mama, kaka, dada, mara tu anapozaliwa kwa lengo la kumtaka mtoto alale. Hutolewa kwa kughaniwa pale mtoto anapobebwa mgongoni au anapopakatwa. Nyimbo hizi zina matumizi mbalimbali na huwaathiri watu wazima. Inaonekana kuwa mama huwa na duku duku lake na ili kuepuka kujisemea peke yake hujiimbia yeye mwenyewe na hutamani kama awepo mtu amsikilize ili apate kumuonea huruma na huonekana kana kwamba anamuimbia mtoto, kumbe mama anapoimba huwa hamshughulikii mtoto kwa

kumuhusisha na maudhui bali huwa mama anajisemea nafsi yake. Mtaalamu huyu ameeleza namna nyimbo zinavyowaathiri watu wazima na kutoa duku duku lao pindi wanapoziimba nyimbo hizo. Mtaalamu huyu ametoa mchango mkubwa kwa utafiti huu na kuonesha ipo haja ya kushughulikiwa kwa kuchunguzwa dhamira za nyimbo bembelezi za watoto.

Othman (2007) anasema tangu enzi, duniani kote wazee huwaimbia nyimbo watoto wao huku wakiwa watoto hao wamebebwa mgongoni au wamewapakata na kuwatikisa kwa uangalifu mkubwa ili walale au watulie. Nyimbo zinazoimbwa zina dhima tofauti tofauti lakini toni zake na viitikio vyake vinafanana katika nyimbo hizo. Viitikio hivyo huwa ni vya sauti ambazo zinaigiza sauti ya kilio au mtu anaehuzunika. Nyimbo hizi hutaja kwa uwazi au kwa kificho malalamiko hayo na huwa zinamrejelea mama wa mwimbaji. Hii hutokea pale mtoto anapolia, kilio ambacho humkumbusha mama huzuni, machungu na mateso ya ulezi, pia hugusia ugumu wa maisha. Nyimbo hizi humtakia dua mtoto akue haraka na awe mtoto mwema ili aje amzike mama yake wakati atakapofariki dunia. Maelezo ya mtafiti huyu yanaonekana kuwa ni dira katika utafiti huu, kwani yamegusia malalamiko yaliokuwemo kwenye nyimbo hizo na namna tendo la nyimbo za watoto lilivyotekelezwa. Pamoja na kugusia dhima tofauti, na sauti za mtu aliehuzunika, lakini upeo wake haukufikia kuchunguza dhamira kwa jamii. Hivyo, utafiti huu umechunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi.

Mulokozi (2003) na Pauline (2009) wameangalia aina mbalimbali za nyimbo katika jamii za kiafrika, pamoja na kuziweka katika makundi tofauti, miongoni mwa makundi hayo ni nyimbo za kubembelezea watoto. Nyimbo hizo huwa zinasimulia

na kuelezea mambo yanayotokea katika jamii, zikiwa na malengo ya kufunza, kuelimisha, kukosoa, na kuburudisha. Kulingana na makundi hayo kwa mujibu wa wataalamu hao, nyimbo za kubembelezea watoto za kimakunduchi zinaingia katika makundi yote yaliyotajwa na wasanii hao kwa sababu nyimbo za kubembelezea watoto kutoka Makunduchi zinazungumzia mambo mengi ya kijamii. Hivyo mawazo ya wataalamu hawa yamemsaidia sana mtafiti katika kuupeleka mbele utafiti huu.

Ali (2013) ametafiti athari za mitindo katika kuibua maudhui mifano kutoka nyimbo bembelezi za Pemba. Ameeleza namna mitindo inavyoibua maudhui kwa kutumia mifano ya nyimbo bembelezi za Pemba, na aliweza kubaini mbinu zitumikazo kusawiri maudhui hayo na wakati huo huo mtoto akafarijika, akanyamza na akapata usingizi. Aliendelea kusema kuwa sauti ya upole, yenye kusihi na viitikio vyake ambavyo hurudiwa rudiwa kwa mahadhi ndio moja ya mbinu zitumikazo katika nyimbo hizo. Mawazo ya mtafiti huyu yamemsaidia sana mtafiti wa utafiti huu katika kuupeleka mbele utafiti huu wa kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi.

2.3 Mkabala wa Kinadharia

Katika sehemu ya pili ya sura hii mtafiti ameonesha nadharia zilizotumika katika kuuongoza utafiti huu. Sengo (2009) anasema nadharia ni muongozo mkuu au wazo kuu au fikra kuu inayotumiwa na mtu au watu au jamii fulani kwa kukabiliana na mazingira yake. Anaendelea kusema nadharia ni mfumo wa mawazo au maarifa yanayofasili taaluma mahsusi kwa kutoa maoni, mtazamo au falsafa juu ya matumizi na taratibu za utafiti. Wafula na Njogu (2007) wanasema nadharia ni istilahi ya kijumla inayomaanisha miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya fasihi

kuifahamu kazi ya fasihi katika vipengele vyake vyote. Nadharia ni maelezo ya jambo linalofungamana na vigezo vilivyowekwa au vinavyozalika kutokana na majaribio ya jambo hilo. Hivyo basi, katika utafiti huu nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na nadharia ya Semiotiki zimetumika katika utafiti huu.

2.3.1 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inajadiliwa na Wamitila (2002), kuwa ni nadharia inayorejelea mitizamo au tabia fulani za usomaji wa matini zinazohusisha uhakiki wa aina mbalimbali ambayo huangaza dhima na majukumu ya msomaji katika matini au kazi za fasihi. Wataalam wanaohusishwa na nadharia hii ni Hawthorn na Margaret Atwood katika miaka ya 1960 mwishoni na 1970 mwanzoni.

Lengo la kimsingi la nadharia hii ni kuwabainisha wasomaji, kuwachunguza pamoja na tendo zima la usomaji. Wahakiki wanaojishughulisha na nadharia hii wanaelekea kuwa, na mtazamo tofauti na ule wa kijadi wa kuiangalia fasihi kama kitu kilichokamilika. Hawa wanaamini kuwa, maana yoyote ya kifasihi inamtegemea kwa kiasi kikubwa msomaji wa kazi hiyo. Msomaji husawiriwa kama mwenye mchango mkubwa katika kubuni maana ya kazi husika ya fasihi. Hii ni sawa na kusema kuwa si rahisi kudai kuwa kuna maana fulani sawa au sahihi zaidi ya kazi fulani ya kifasihi kwa msomaji. Wasomaji wanaweza kuvifasiri vipengele vya kiisimu na kisanaa kwa namna mbalimbali. Tofauti hizo za maana huweza kusababishwa na vipengele

mbalimbali vya kimsingi vinavyounda Mwitiko wa Msomaji, tofauti kati ya ubaki wa matini husika na hisia za kibinafsi za msomaji anayehusika na utofauti wa namna matini inavyoelekeza au kutatiza Mwitiko wa Msomaji. Sifa hizi ndizo zinazozua usomaji mzuri au usomaji mbaya wa kazi ya fasihi inayohusika.

Hata hivyo matini za kifasihi huwa na sifa moja inayohusiana, kwani huwezesha kuwepo kwa maana au fasili mbalimbali za kazi moja ya fasihi. Kimsingi tunakubaliana na mawazo ya nadharia hii kwani yanampa msomaji uhuru wa kuweza kuisoma, kuielewa na kuihakiki kazi ya fasihi kwa kadri ya uelewa na tajriba ya msomaji husika kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii.

- Pamoja na kuwa nadharia hii inatumika katika kuzichambua na kuhakiki kazi za fasihi. Wataalamu wa nadharia hii wanasema kuwa kiini cha uhakiki huzoofisha msingi mkuu wa uhakiki mpya hii ni kutokana kuwa matini ya kifasihi ni kitu kinachojitegemea na ambacho huweza kuangaliwa bila kuhusishwa na muktadha. Wanaendelea kusema kuwa wahakiki wenye muelekeo huu wanaamini kuwa maana ya kazi yoyote ya kifasihi inamtegemea kwa kiasi kikubwa msomaji wa kazi hiyo. Hii ina maana kuwa ni vigumu kudai au hata kusema kuwa kuna maana fulani sawa na sahihi ya kazi fulani ya kifasihi kwa msomaji. Wasomaji wanaweza kufasiri vipengele vya kisanaa kwa namna mbalimbali hivyo hupelekea kupatikana kwa tofauti, miongoni mwa tofauti hizo ni kama:
- Kuna vipengele vya kimsingi mbalimbali ambavyo huunda Mwitiko wa Msomaji.
- Ipo tofauti kati ya ubaki wa matini husika na hisia za kibinafsi za msomaji anaehusika.

- Matini husika inaweza kuwa tofauti kwa namna inayoelekeza au kutatiza Mwitiko wa Msomaji. Sifa ambayo inazua usomaji mzuri au usomaji mbaya kwa kazi inayohusika.

Nadharia hii ilipata mashiko zaidi mwishoni mwa miaka ya sitini na sabini baada ya kuwekewa misingi yake na maprofesa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Constance Ujerumani, walisisitiza uchunguzi mpya kuhusu usomaji na upokezi wa matini za kifasihi. Nadharia hii imemsaidia mtafiti kupata maana mbalimbali za matini zilizotumika katika fasihi kulingana na mtazamo wa mtu binafsi. Nadharia hii ilionekana kuwa inaweza kufikisha lengo la utafiti huu, sababu kubwa ni kwamba lengo la utafiti huu ni kuchunguza dhamira mbalimbali zilizojitokeza katika nyimbo bembelezi za watoto zilizoteuliwa. Kwa hiyo, kwa kutumia nadharia hii mtafiti aliona kuwa imeweza kufikia lengo hili. Kama ilivyojadiliwa hapo awali kuwa nadharia hii imejikita zaidi katika kuona mwitiko anaoupata msomaji baada ya kusoma kazi fulani ya kifasihi katika kujenga maana ya kazi hiyo. Kwa hiyo, mtafiti aliona kuwa nadharia hii itakidhi malengo ya utafiti huu na kuuongoza katika kuchunguza, kuchambua na kujadili data za utafiti huu ambao umejikita katika kuchunguza dhamira za nyimbo bembelezi mifano kutoka Makunduchi. Kwa maana hiyo, nadharia hii imemsaidia mtafiti katika uchambuzi wa lengo la kwanza sambamba na hili mtafiti aliona ipo haja ya kuwa na nadharia ambayo itakuwa na kazi ya uchambuzi wa lengo la pili la utafiti katika kukidhi malengo ya utafiti huu. Kwa hiyo, katika utafiti huu wa kuchunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto ilitumika nadharia ya Semiotiki kwa mujibu wa lengo la pili.

2.3.2 Nadharia ya Semiotiki

Ferdinand de Saussure na Charles Pierce ni waasisi wa nadharia hii ya Semiotiki. Saussure katika nadharia hii ameeleza dhima ya ishara katika jamii na Pierce amezungumzia maana halisi ya lugha ya ishara inavyohusiana kimantiki na utamaduni wa jamii fulani kwa madhumuni ya kutoa maana maalum. Blamires (1991) amewanukuu Geoffrey, Hill, Paul na Hold wanazuoni wa Chuo Kikuu cha Yale, wakisema matini moja yaweza kuwa na fasili nyingi zinazolingana au kukinzana na zote zikakubalika.

Wamitila (2002) anasema nadharia hii imetumika sana katika uchambuzi wa kazi za kifasihi, ambapo inashughulikia ishara na uashiriaji. Ishara zinazojitokeza katika kazi za kifashi huundwa na mtunzi (msanii) kwa kuzingatia muktadha wa jamii wa kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. (Wamitila ameshatajwa) anaeleza kwamba, katika lugha kuna vitu viwili, ambavyo ni kitaja (a signifier) yaani umbo ambalo alama inachukua na kirejelee (a signified) yaani maana iwakilishwayo na alama hiyo. Kutokana na maelezo haya tunapata uelewa kuwa, kuna kitaja na kirejelee ambapo mahusiano ya viwili hivyo ni ya kubuni tu, hutegemea utamaduni wa jamii husika. Inawezekana kabisa ikawa hakuna uhusiano kati ya kitaja na kirejelee, lakini kama wanajamii wamekubaliana juu ya matumizi yake basi hutumika na huelewana miongoni mwao.

Nadharia ya Semiotiki imejengwa kwa mihimili mitano ikiwa ndio misingi yake katika kuzifumbua ishara zilizotumika katika kazi ya fasihi. Misingi hiyo ni muktadha, ujumbe, msemaji, mpokeaji na lugha.

Barthes (1994) anaeleza kwamba, kuna aina tano za misimbo zinazotumika katika kazi ya kifasihi ambazo kwa pamoja huunda nadharia ya Semiotiki. Mhakiki huyu

alizuka na dhana hii kupendekeza jinsi bora ya kuisoma kazi ya kifasihi au matini ya kifasihi. Lengo la Barthes (ameshatajwa) ni kuivunja matini ya kifasihi kwenye sehemu ndogo ndogo alizoziita leksia. Hivi ni kama vitengo vidogo vya kisomaji ambavyo vina urefu sawa. Kwa mujibu wa mawazo yake, kila leksia hudhihirisha misimbo au kaida fulani ambazo huwa muhimu katika kuifasiri. Aina tano kuu za misimbo imeishia kuitwa ‘misimbo ya usomaji’ na ni nguzo muhimu katika nadharia hii. Aina hizo za misimbo ni msimbo wa kimatukio, kihementiki, kiseme, kiishara na kirejelezi.

Msimbo wa matukio: unahusu jinsi matukio yanavyoungana na kushonana kutokana na kusababishana au kuathiriana katika mashairi husika (Omari, 2015). Imezoeleka kuona wataalamu wengi wa fasihi ya Kiswahili wakihusisha dhana ya matukio na vitushi na tanzu za riwaya na tamthilia kuliko ushairi (Njogu na Chimera, 1999). Hata hivyo tunafahamisha kwamba, hata katika ushairi wa Kiswahili ambamo ndani yake kuna kipera cha nyimbo kuna matukio mbalimbali yanayotokea hususani katika nyimbo bembelezi za watoto, ambapo kunapatikana hadithi au simulizi fulani yanavyofuatana na jinsi msomaji anavyouunda na kuuelewa msuko wa kazi hiyo kwa kuangalia jinsi matukio hayo yanavyofuatana kiathari.

Msimbo wa kihementiki: unahusu taharuki na unajulikana na baadhi ya wahakiki kama msimbo wa kusimulia au kutamba hadithi. Kimsingi, msimbo wa kihementiki humfikirisha msomaji juu ya kile anachokusudia kukisoma au kukitafiti. Katika utafiti wetu tuliongozwa na msimbo huu katika kujua kilichokuwa kinataka kusimuliwa na wasanii. Kwa mfano wimbo wa dume kongwe kupitia wimbo huu mtu hupata taharuki na kutaka kuelewa hilo dume kongwe limefanya nini? Na ndio

lipi hilo? Katika kutaka kufahamu majibu ya maswali haya msomaji hulazimika kuuwimba wimbo mzima ili apate majibu yake.

Msimbo wa kiseme: kwa asili unatokana na neno sema. Wamitila (2002) anaeleza kwamba neno sema hutumiwa kuielezea elementi nasibishi ya kisemantiki, hizi ni elementi ambazo zinatuwezesha kupata picha fulani, kutokana na viashiria fulani hupelekea kuelewa sifa kamili ya jambo, tukio, hali au mhusika fulani wa kazi ya fasihi. Kupitia msimbo huu tulinasibisha baina ya vitu, watu, nyakati na hali zinazojitokeza katika nyimbo bembelezi za watoto na kuhusianisha na hali iliopo katika jamii.

Msimbo wa kiishara: ni msimbo muhimu katika usomaji na uhakiki wa kazi za kifasihi kwani unahusishwa na jinsi ambavyo wasomaji wanavumbua maana za kiishara katika kazi ya kifasihi (Omari, 2015) katika hili, mfano mzuri unaonekana katika wimbo wa “Msikiti wa jibondo” linapopatikana maneno “kandili, nyaraka” kwenye mstari wa kwanza na wa pili wa wimbo usemao:

Msikiti wa jibondo kandili mbili zawaka

Wamo wasomaji vyuo na waandikao nyaraka

Tunapoliangalia maneno kandili, nyaraka tunaona kuwa yametumika kiishara katika kumaanisha mambo kadhaa ambapo msomaji atalazimika kwa kina maneno haya ili aweze kuipata maana iliyokusudiwa.bila shaka yoyote, ishara hizi ni sehemu ya vipengele vya mbinu za kisanaa wanavyotumia wasanii katika kusawiri dhamira za nyimbo bembelezi za watoto.

Msimbo kirejelezi: huu unajengwa kutokana na viashiria vya utamaduni unaorejelewa katika kazi inayohusika ya kifasihi. Wamitila (2002) anaeleza kwamba,

urejelezi huu huunda uhalisi mahususi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo kuipa kazi fulani nguzo za kiutamaduni. Mfano mzuri wa msimbo huu unapatikana katika wimbo uitwao "kidau" msanii anasema:

Kile kidau kijacho nnageza mna changu,
Mna mkufu nitunge kadiri ya shingo yangu,
Siuvai siutupi wala simkii mwenzangu,
Tamka mama mzazi msiri wa mambo yangu,
Bwana wewe sikwebu waninyezeza nini kwangu?

Tunapoimba wimbo huu tunakutana na maneno "kidau, mkufu". Maneno haya ni ya kiutamaduni yenye kurejelea mambo mbalimbali katika jamii. Muimbaji anapokutana na maneno haya ya kiutamaduni huweza kupata picha ya haraka juu ya kile kinachozungumzwa na mwimbaji (msanii).

Kwa kuwa utafiti huu umejiegemeza sana katika kuchunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto, nadharia ya Semiotiki imesaidia kwa kiasi kikubwa katika kufikia kilele cha kukamilisha uchunguzi na uchanganuzi wa data za utafiti huu. Hii ni kwa sababu kuwa msingi wa nadharia ya Semiotiki katika kuchambua ishara ni kuchunguza matumizi ya muktadha wa ishara, ujumbe, aina ya msemaji, aina ya mpokeaji na wepesi au uzito wa lugha iliyotumika kulingana na aina ya mpokeaji au msemaji na pia nguzo tano zilizoijenga nadharia hii zimeweza kukamilisha lengo la pili, ambalo lilihusiana na ubainishaji wa mbinu za kisanaa zilizotumiwa na wasanii wa nyimbo bembelezi za watoto katika kufikisha ujumbe kwa jamii.

2.3 Pengo la Maarifa

Kama tulivyoona katika mjadala wa hapo juu, tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu kuchunguza nyimbo bembelezi za watoto kwa watafiti tofauti. Hata hivyo kwa upeo wa mtafiti wa utafiti huu, bado hatujapata uthibitisho wa kazi ya utafiti ambayo imechunguza dhamira ya nyimbo bembelezi za watoto: mifano kutoka Makunduchi. Hivyo basi, utafiti huu umejaribu kuziba pengo hilo kwa kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi.

2.4 Hitimisho

Katika sura hii imejadili kuhusu mapitio ya maandiko mbalimbali kuhusu nyimbo kwa jumla, dhamira za nyimbo na tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu nyimbo bembelezi za watoto. Aidha katika mijadala hiyo, mtafiti ameweza kubaini pengo la kimaarifa na kuonyesha hitaji lililopelekea umuhimu wa kufanyika kwa utafiti huu. Vile vile sura hii imejadili kiunzi cha nadharia kwa kutalii nadharia ambazo zilionekana zinaweza kuongoza utafiti huu. Katika mjadala wa kiunzi cha nadharia, utafiti huu umejadili mihimili ya nadharia hizo, ubora na upungufu wake katika kuchunguza, kuchambua na kujadili data za utafiti huu. Aidha, kwa kufanya hivyo utafiti huu uliweza kuchagua nadharia ya Mwitiko wa Msomaji pamoja nadharia ya Semiotiki na kuonyesha uthabiti wa nadharia hizo, sababu za kuzichagua na namna zilivyotumika katika utafiti huu. Sura inayofuata inahusu mbinu za utafiti.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Kothari (2004) anasema Sura hii imewasilisha mbinu mbalimbali za utafiti zilizomsaidia mtafiti katika kupatikana kwa data kwa kuangalia vipengele mbalimbali ambavyo vimeunda na kukamilisha sura hii. Vipengele vilivyobainishwa katika sura hii ni pamoja na eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, aina ya utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji. Aina ya data iliyokusanywa, mbinu za kukusanya data, mbinu za kuchambua data na maadili ya utafiti ni miongoni vya vipengele vilivyokamilisha sura hii na kumalizia na hitimisho.

3.1 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti unafanyikia kulingana na vile mtafiti alivyopendekeza ili kupata data za kujibu maswali yake ya utafiti (Creswell, 2009). Utafiti huu umefanyika umefanyika Zanzibar, kisiwa cha Unguja, Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Kusini kama ilivyobainishwa na Mlacha na Hurskainen (1996) eneo la

kijiografia la utafiti huu, utafiti huu umeshughulikia kuchunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi, ambapo mtafiti amehusisha mitaa minne tu ya kijiji hicho nayo ni Kiongoni, Kumbini, Kajengwa na Mtaandani, maeneo yote haya kwa pamoja yameweza kumpatia mtafiti data stahiki za utafiti huu na maeneo haya ndio ambayo vinapopatikana vituo vya kulelea watoto. Eneo la Mkoa wa Mjini Magharibi limeteuliwa kwa sababu ndimo mnamo patikana maktaba ambazo mtafiti ameweza kukusanya data za utafiti huu na kutoa data stahiki kwani ndipo pahala muafaka paliposaidia kupata data za msingi za utafiti huu. Eneo la utafiti huteuliwa kulingana na nia kuu ya mtafiti na kwamba eneo hili ndilo lililoweza kutoa data za kukamilisha lengo la utafiti. Kwa upande wa nadharia, utafiti huu umehusisha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na nadharia ya Semiotiki.

3.2 Usanifu wa Utafiti

Kothari (2004) anasema usanifu wa utafiti ni mpangilio maalum unaoonesha namna na jinsi utafiti utakavyofanyika ili kuwezesha kujibu maswali ya utafiti husika. Usanifu wa utafiti huu ni uchunguzi kifani ambapo nyimbo bembelezi nane (8) zimeteuliwa na kuchunguzwa ili kubainisha namna zinavyozungumzia dhamira katika jamii ya leo kupitia mbinu mbalimbali za kisanaa. Pia utafiti huu umefanyika katika Mkoa wa Mjini Magharibi ambapo ndipo zilipopatikana maktaba zilizosaidia kupatikana kwa data za upili na katika Mkoa wa Kusini katika Wilaya ya Kusini katika kijiji mtaa wa Kajengwa, Kumbini, Mtaandani na Kiongoni ambapo ndipo watafitiwa walikopatikana. Creswell (2009) anasema kuwa uchunguzi kifani hutoa fursa ya kuchunguza jambo kwa undani zaidi na kuhusisha vipengele mbalimbali

vilivyounda au kujenga jambo hilo, kwa hivyo uchunguzi kifani umemsaidia mtafiti katika kuchunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto zilizoteuliwa

3.3 Aina ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo ambao umehusisha aina ya utafiti wa maktabani na maskanini.

3.3.1 Maktabani

Aina ya ukusanyaji wa data maktabani huhusisha data kupitia katika maandiko na machapisho mbalimbali kama vile vitabu, magazeti na matini zisomwazo ambazo hutongolewa na pia zilizochapichwa (Kothari, 2008). Katika kupitia maandiko haya uchambuzi hufanywa kwa mujibu wa malengo ya mtafiti ili kuweza kukamilisha utafiti husika kwa kuangalia matini mbalimbali. Aina hii inahusisha kupata habari za kina kwa kusoma maandiko na kuangalia taarifa katika vyanzo mbalimbali. Hivyo mtafiti wa utafiti huu aliangalia magazeti, vitabu, makala, tasnifu, nyaraka na taarifa mbalimbali zilizomo mtandaoni.

3.3.2 Maskanini

Ni aina ya utafiti ambao mtafiti huteuwa wasailiwa na vibadilika na hatimae kupima tabia zinazojitokeza katika hali fulani (Buliba na wenzake). Kwa hiyo utafiti huu umefanyika katika Mkoa wa Kusini katika Wilaya ya Kusini kupitia vijiji vya Kajengwa, Kiongoni, Kumbini na Mtaandani. Sehemu ambayo mtafiti ameweza kupata wasailiwa kama vile wazee ambao wana uelewa, ujuzi na uweledi wa kuimba nyimbo hizo ambao walikuwa wakizitumia katika ujana wao walipokuwa wakilea watoto, wazazi wenye watoto ambao na wao kwa kiasi kikubwa wana ujuzi wa kuzitumia nyimbo hizo wakati wa kubembeleza watoto wao.

3.4 Kundi Lengwa

Cooper (1989) na Varis (1990) wanafasili kundi lengwa ni wanachama au walengwa wote au hata mtu mmoja, kundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake, katika utafiti huu walengwa walikuwa ni wazee wa kike na wazazi wenye watoto wachanga ambao ni wakaazi wa kijiji cha Makunduchi ambao ni walezi na wazazi na pia ni watumiaji wa asili wa lahaja ya kimakunduchi, waliokuwa wakitumia nyimbo bembelezi za watoto ambapo kwa sasa hawatumii sana kwa vile zimeingiliwa na utandawazi. Nyimbo hizo zilikusanya dhamira tofauti, kwani hazikuwalenga watoto tu bali pia zilikuwa na dhamira nyengine kwa jamii.

3.5 Sampuli Na Usampulishaji

Usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu kutoka kundi lengwa ili litumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwa kuwa sio rahisi kutafiti kundi lengwa zima (Enon 1998, Spata 2003, Bryman 2004 na Walliman 2011). Zipo mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa katika uteuzi wa sampuli, lakini sampuli ya utafiti huu imetumia mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu.

3.5.1 Sampuli

Sampuli ni kitu au vitu kati ya vingi vya aina ileile vinavyochukuliwa kama mfano mzuri wa vitu hivyo (TUKI, 2004). Homby (2006) anadai kuwa sampuli ni jumla ya washiriki walengwa kutoka katika kundi kubwa ambalo mtafiti amekusudia kulifanyia utafiti ili kupata taarifa zihusuzo mada yake na hatimaye kupata hitimisho. Hata hivyo, Kothari (2004) ameeleza kuwa sababu ya kuteuwa sampuli katika sayansi ya jamii ni kuokoa muda, gharama na nguvu kazi wakati wa kufanya utafiti.

Hivyo haikuwa rahisi kwa mtafiti kuweza kuwatafiti waimbaji wote wa nyimbo bembelezi za watoto, hivyo mtafiti aliteuwa wazee wanane 8, wawili kwa kila mtaa ambao ni wenye ujuzi na wanazielewa nyimbo bembelezi za watoto, idadi hii ilitokana na kukosekana kwa wazee wengi ambao wana kumbukumbu juu ya nyimbo za watoto zinazotakiwa. Na pia mtafiti aliteua wazee na walezi wenye watoto watano kwa kila mtaa idadi ya walezi hao ni 20, hivyo kulikuwa na jumla ya watafitiwa 28 kutoka katika mitaa minne iliyoteuliwa.

3.5.2 Usampulishaji

Brayman (2004) anasema usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kikundi cha watu au vitu

ili kitumike katika utafiti kama ni kiwakilishi cha kundi linalotakiwa kufanyiwa utafiti kwani si rahisi kuwatafiti kundi zima. Zipo mbinu mbalimbali za usampulishaji hivyo mtafiti alitumia mbinu zifuatazo ili kulipata kundi dogo lililowakilisha jamii kubwa ya watafitiwa. Hivyo katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalum.

3.5.3 Uteuzi Wa Madhumuni Maalumu

Uteuzi wa sampuli kwa kutumia kigezo cha madhumuni maalumu ni uteuzi wa sampuli kwa kuzingatia sababu mahususi. Katika mbinu hii ya uteuzi wenye madhumuni maalumu, sampuli huteuliwa kwa kuzingatia vigezo maalumu ambavyo vitakuwa na uhusiano na maswali ya utafiti ili yaweze kujibiwa kwa urahisi na ukamilifu (Powell na Conway, 2004). Kombo na Tromp (2006), wanasema, ni uteuzi ambao mtafiti kwa makusudi hulenga kuteua kundi la watu ambao anaamini kuwa ni

raslimali anayoitegemea katika utafiti wake. Mbinu hii humpa mtafiti uhuru katika kuteua sampuli itakayowezesha kujibu maswali ya utafiti (Neuman, 2006).

Mtafiti alitumia mbinu hii kuwateua wazee wenye uweledi na ujuzi wa kuimba nyimbo bembelezi za watoto ikiwa pamoja na wenye watoto wachanga, aliwateua watafitiwa hao kwa vile alijua kuwa wao ndio watu maalumu wanaoweza kumpatia data zinazohusu nyimbo bembelezi za watoto.

3.6 Aina ya Data Iliyokusanywa

Utafiti huu umekusanya data za aina mbili. Data za msingi na data za upili.

3.6.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile data halisi ambazo hazijapata kukusanywa na mtafiti mwengine kwa madhumunii ya kujibu maswali ya utafiti (Kothari, 2004). Hivyo data za msingi za utafiti huu zimekusanywa kutoka katika vyanzo vikuu viwili. Chanzo cha kwanza kilihusisha data zilizokusanywa kutoka nyimbo teule. Na chanzo cha pili data zilikusanywa kutoka kwa watafitiwa.

3.6.2 Data za Upili

Data za upili ni zile data ambazo tayari zimekwisha kusanywa kutoka kwa watafiti wengine na kuchapishwa au kuandikwa katika kujibu maswali ya tafiti zao. Data za upili zinapatikana katika maktaba kwa kuangalia na kukusanya maandishi mbalimbali yanayohusu mada ya utafiti huo, mtafiti alikusanya data kutoka katika vitabu vya wataalamu mbalimbali, makala, maajarida, tafiti zilizopita na vipeperushi mbali mbali kwa lengo la kukamilisha utafiti huo. Young (1984) anasema data za upili ni aina ya kukusanyasa data mezani bila ya kuwatafuta au kuwafuata watafitiwa na kuwahoji au kuwafanyiwa usaili.

3.7 Mbinu za Kukusanya Data

Mbinu ni njia ya kufanyia jambo kwa urahisi (BAKITA 2010). Mtafiti ametumia mbinu ya kupitia machapicho, ushuhudiaji, kusikiliza na mahojiano. Mtafiti ametumia mbinu ya kupitia machapicho mbalimbali yanayohusu nyimbo, dhamira za nyimbo na mbinu za kisanaa zilizomo ndani ya nyimbo hizo, ametumia mbinu ya ushuhudiaji katika kushiriki kama mtazamaji, katika mbinu ya mahojiano imemsaidia kuchunguza na kukusanya nyimbo bembelezi mbalimbali kwa kuwahoji wazazi na walezi, katika mbinu ya kusikiliza amewasikiliza mabibi ambao hawajui kusoma wala kuandika wakati akiwauliza maswali.

3.7.1 Mbinu ya Kupitia Machapisho Mbalimbali

Kothari (2004) amefasili mbinu hii na kusema inajumuisha uchambuzi wa maandiko kama vile vitabu, magazeti na matini zisomwazo ambazo hutongolewa na pia zilizochapishwa. Uchambuzi huu hufanywa kwa ajili ya kuangalia ujumbe muhimu uliomo kwenye matini husika. Njia hii inahusisha kupata habari za kina kwa kusoma maandiko na kuangalia taarifa katika vyanzo mbalimbali. Maandiko yanaweza kuwa vitabu, magazeti, makala, hotuba, matangazo, picha na mengine mfano wa hayo. Mtafiti alipitia maandiko mbalimbali na kupata nukuu na ufafanuzi wa dhana, nadharia na data za kutosha zilizohusiana na utafiti wake kulingana na mada, malengo na mipaka ya utafiti. Mtafiti alisoma na kupitia marejeleo kama vile tasnifu, majarida, vitabu na tovuti kutoka mtandaoni.

3.7.2 Mbinu ya Ushuhudiaji

Ushuhudiaji ni mbinu mojawapo ya ukusanyaji wa data ambayo mtafiti aliitumia katika utafiti huu. Katika njia hii mtafiti hulazimika kwenda katika eneo husika na kushuhudia kile anachokitafiti (Mulokozi, 2010)**.** Njia hii ilitumika kwa kuhudhuria katika baadhi ya sehemu zenye wazee wenye watoto. Sehemu hizi mtafiti alichunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto na kuwaangalia wabembelezaji yeye akiwa kama ni mtazamaji.

3.7.3 Mbinu ya Kusikiliza

Mbinu hii ya kusikiliza ilifanywa na mtafiti kwa kuuliza maswali yaliyokuwa yanahusiana na mada inayoshughulikiwa. Mathalani, maswali yalioulizwa ni Je, siku hizi nyimbo za kubembelezea watoto zinaendelea kutumika au hazitumiki? Mbona wazazi hawawaimbii watoto wakati wanapowabembeleza? Watafitiwa walijibu na kutoa sababu zao, moja ni kuwa zinaanza kusahaulika na hao wanaozijua hawaziimbi.

3.7.4 Mbinu ya Mahojiano

Mbinu ya usaili au mahojiano ilitumika katika utafiti huu ili kupata data za msingi za utafiti. Kombo na Tromp (2006) Cohen na wenzake (2000) wanasema mahojiano ni mbinu ya ukusanyaji data kwa njia ya mazungumzo ya moja kwa moja baina ya mtafiti na mtafitiwa. Kothari (2004) anabainisha kuwa njia ya usaili huwepesisha upatikanaji wa data kwa kuwa inawajumuisha wanaojua kusoma na wasiojua pia. Aidha, husaidia kupata data muhimu zaidi kwa kuwa hutoa fursa zaidi kwa mtafiti kuuliza masuali ya ziada. Mahojiano yalifanyika kwa Wazee nane wenye kuzifahamu nyimbo bembelezi za watoto kutoka mitaa minne iliyoteuliwa kutoka katika kijiji cha Makunduchi. Pia, ilitumika kwa Wazazi wanne kutoka kila mtaa. Mbinu hii iliwezesha kupatikana nyimbo za kubembeleza watoto kwa kiasi kikubwa.

3.9 Mbinu za Kuchambua Data

Uchambuzi wa data kwa mujibu wa Kothari (2013), ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo imesaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Wakiunga mkono hoja hii Bogdan na Biklen (1992), wakinukuliwa na Omari (2011), wanaeleza kuwa, hii ni hatua muhimu sana katika kutafuta majibu ya tatizo la utafiti husika. Zipo mbinu mbalimbali za uchambuzi wa data lakini data za utafiti huu zilichambuliwa kwa njia ya maelezo. Uchambuzi wa kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambayo humruhusu mtafiti kusikiliza au kusoma kisha kuelewa maudhui yake. Kwa muktadha huu mtafiti alitumia mbinu hii kwa kusikiliza nyimbo zilizoimbwa na watafitiwa na kuchunguza dhamira zilizojitokeza katika nyimbo bembelezi za watoto pamoja mbinu za kisanaa katika kusawiri dhamira za nyimbo hizo.

3.10 Maadili ya Utafiti

Miongoni mwa vitu muhimu vinavyopasa kuzingatiwa na mtafiti yoyote ni maadili ya utafiti (Kumar, 1999), akinukuliwa na (Omary, 2015). Vipengele vinavyohusika katika maadili ya utafiti ni kuomba na kupewa kibali cha kufanyia utafiti na kutunza siri za taarifa, ridhaa ya watafitiwa pamoja na uchukuaji wa picha yalizingatiwa kikamilifu. Uzingativu wa vipengele hivi huufanya utafiti kutoa matokeo sahihi ya utafiti husika na kuweza kuaminiwa kitaaluma kwa kuyazingatia maadili hayo kabla na baada ya kukusanya data. Katika kuhakikisha kwamba utafiti huu unatoa matokeo stahiki tulizingatia vipengele vyote vya maadili ya utafiti tulivyovitaja sehemu hii.

3.11 Hitimisho

Sura ya tatu imeelezea juu ya vipengele vya mbinu za utafiti, vifaa na mambo mbalimbali yaliyohusishwa na kazi ya ukusanyaji na uchambuzi wa data. Aidha, imeeleza mbinu zilizotumika katika utafiti huu ni uwandani, kusikiliza na mahojiano. Kwa upande wa vipengele vingine ni sampuli na usampulishaji, mbinu ya uchambuzi wa data, mkabala wa kimaelezo, sura hii imeelezea mpango na walengwa wa utafiti. Pia, imeonesha jamii ya watafitiwa, eneo la utafiti, ukusanyaji na uchambuzi wa data, na kipengele cha mwisho ni miiko na maadili ya utafiti. Sura inayofuata inahusu uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA

4.0 Utangulizi

Sura hii imewasilisha, uchambuzi na mjadala wa data. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto. Malengo mahsusi ya utafiti huu yalikuwa mawili; kuchambua dhamira zinazopatikana ndani ya nyimbo bembelezi za watoto na kubainisha mbinu za kisanaa zilizotumiwa na wasanii katika kusawiri dhamira zilizopatikana ndani ya nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi. Sambamba na malengo mahsusi, utafiti huu umejibu maswali mawili nayo ni; Ni dhamira zipi zinazopatikana ndani ya nyimbo bembelezi za

watoto? na mbinu zipi za kisanaa zinazotumiwa na wasanii katika kusawiri dhamira zilizopatikana katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi?.

Uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa matokeo katika utafiti huu vimepangwa kwa mtiririko wa kufuata malengo mahsusi. Sehemu ya kwanza imechunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi, sehemu ya pili imeangalia mbinu za kisanaa zinazotumiwa na wasanii katika kusawiri dhamira zinazopatikana katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi.

4.1 Kubainisha Dhamira Zilizojitokeza Katika nyimbo Bembelezi

Katika sehemu hii mtafiti amefanya uchambuzi wa dhamira zinazojitokeza katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi ili kuonesha namna dhamira zinavyoendana na hali halisi ya maisha katika jamii. Wamitila (2008), anaeleza kwamba, watunzi wa kazi za fasihi ni watu ambao huyachukua matukio na visa vinavyotokea katika jamii zao na kuviwasilisha kiubunifu katika riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Kubuni haina maana ni kudanganya, bali ni kuwasilisha dhamira kwa kutumia mbinu za kisanaa na hususani katika fasihi, hujulikana kama fani ili kuleta hamu na hamasa kwa msomaji kuvutiwa kuisoma kazi husika na kuzipata barabara dhamira zilizolengwa na mtunzi husika. Mifano ya nyimbo bembelezi za watoto kutoka Makunduchi ni miongoni mwa kazi za kifasihi ambazo zimawasilisha dhamira zinazohusu maisha ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Kwa mujibu wa watafitiwa, wameeleza kwamba nyimbo bembelezi zimekusanya dhamira mbalimbali kulingana na mbembelezaji alivyokusudia, ama kuhimiza kitu, au kusemea jambo kwa jamii, au zimejikita katika kufikisha ujumbe husika pale kinapotendeka kitendo chenyewe cha ubembelezaji. Kwa mujibu wa maelezo ya

watafitiwa hao nyimbo bembelezi zimesheheni dhamira tofauti kama dhamira ya mapenzi, malezi, elimu, nafasi ya mwanamke, athari za uzee, uonevu, usaliti, utunzaji siri, kukinai, ukweli, ubaguzi, utamaduni, uchumi, chuki, uchoyo, ubaya, kuomba msamaha, kusameheana kukiri kosa na wizi.

4.1.1 Mapenzi

Mapenzi ni hisia nzito ya moyoni inayomfanya mtu avutiwe, athamini na ajali mtu kitu au jambo (kamusi la Kiswahili Bakiza, 2010). Dhamira ya mapenzi ni miongoni mwa dhamira maarufu kati ya zote zinazopatikana katika kazi ya fasihi kama vile riwaya, tamthilia, ushairi na hadithi fupi pamoja na kazi nyenginezo (Omari, 2014). Dhamira hii imekuwa ikiwasilishwa kwa namna mbalimbali kulingana na madhumuni ya kila mwandishi anapoandika kazi yake ya fasihi. Njogu na Chimerah (1999) wanasema mapenzi katika jamii hutazamwa kwa mtu na mpenzi wake kama mume na mke, mtu na wazazi wake, mtu na jamii yake, na mtu na taifa lake

Kwa mfano, Shaaban Robert ni miongoni mwa watunzi mashuhuri katika fasihi ya Kiswahili ambao wanaheshimika sana kwa kuyaona mapenzi kwa mapana na marefu huku akiyahusisha mapenzi na vitu kama vile, suala la ukweli, upendo, amani, utulivu, heshima busara na hekima miongoni mwa wanajamii. Maelezo ya kina kuhusiana na mambo haya ameyaeleza vizuri katika kazi zake mbalimbali lakini katika *Mapenzi Bora* ndimo ambapo amemakinika zaidi suala hili pia anaona mapenzi ndiyo yanayowaunganisha walio hai na wafu. Kiango (2012) anamuelezea Shaaban Robert katika kuelezea mapenzi kwamba ndio dawa bora ya kuondoa mambo yote yaliyo mabaya baina ya wanadamu. Anaendelea kusema kuwa chuki, choyo, ubaguzi, migogoro vyote hivi vitamalizwa na mapenzi.

Kwa mujibu wa watafitiwa wa nyimbo bembelezi za watoto, wasanii wa nyimbo hizo wameelezea mapenzi kwa upeo wa hali ya juu kwa kuonyesha mapenzi ya dhati, baina ya mama na watoto wao, na pia mapenzi baina ya mtu na mpenzi wake.

4.1.2 Mapenzi ya Dhati

Kazi nyingi za fasihi zimeonesha mapenzi ya dhati baina ya mke na mume na baina ya wazazi na watoto wao. Mfano mwandishi Said Ahmed katika kitabu chake cha Tata za Asumini (1990) ameonyesha mapenzi ya dhati ya wazazi kwa mtoto wao. Asumini ameoneshwa mapenzi na wazazi wake kwa kumpa malezi yalio mazuri na kumjengea heshima katika makuzi yake. Vile vile mwandishi amemuonesha mhusika Seif juu ya mapenzi ya dhati aliyonayo kwa Asumini jambo ambalo lilimuathiri hata kufikia kuacha chuo baada ya Asumini kukimbia Chuoni. Katika nyimbo bembelezi za watoto yameonekana mapenzi ya dhati kwa mama na mtoto wake, au kwa mtu na mpenzi wake. Mapenzi haya yanajitokeza katika wimbo ufuatao wa Usilie kwa kusema:

Usilie usilie ukaniliza na mie

Machozi yako yatue haja hafwa unililie

Ujibwage bwage na chiiii watu wakushikilie

Wenye machozi karibu nao wakusaidie

Anlele mwanagu anlelele

Katika dondoo hili wasanii wameonesha mapenzi ya dhati ya mama na mtoto ambayo yamejitokeza katika wimbo huu. Mapenzi yalioneshwa hapa ni kwamba mama anamhurumia mtoto wake yanapomtokezea matatizo kwani anampa maliwaza kwa kumueleza na kumfahamisha ili aepukana na matatizo hayo, jambo ambalo madhara yake yatakuwa makubwa mpaka kwa mama yake kwa kusema “*usilie usilie*

ukaniliza na mie". Maneno haya hayakusemwa kwa ajili ya kumchombeza mtoto bali walikuwa na dhamira ya kumuonesha mapenzi mwanawe kwamba tatizo lolote linalompata mtoto kimbilio ni mama mzazi, kwani tegemeo kubwa la mzazi kumuona mwanawe akiwa katika furaha, faraja na mapenzi, bali mzazi yeyote hapendelei kumuona mwanawe akiwa katika hali ya matatizo. Vile vile dhamira hii tunaiyona katika riwaya ya *Kiu* (2009) mwandishi anamuonesha mhusika Cheusi ambaye ni mama wa Bahati akimliwaza mwanawe baada ya kupata matatizo kutoka kwa mhusika Iddi. Aidha, katika wimbo huo wasanii wanaonesha baadhi ya wakati watoto wanatakiwa kuficha hisia zao kwa wazazi kwani wanasema "*machozi yako yatuwe haja hafwa unililie*". Hapa wasanii wanaonesha matatizo hayatokezei upande mmoja tu bali hutokezea kwa pande zote mbili kwa mtoto na kwa mama. Hivyo basi, wimbo huu unadhihirisha mama nae akitokewa na matatizo mliwazaji ni mtoto, mmoja kati ya wawili hawa akiondoka anaebakia anaachwa na hudhuni kubwa kama unavyoendelea wimbo huu kusema "*machozi yako yatue haja hafwa unililie, ujibwage bwage na chii watu wakushikilie"* katika mstari miwili hii inaonyesha kwamba akiondoka mama akimwacha mtoto, hudhuni nyingi humpata mtoto huyo. Bali watatokezea wengine ambao watakuwa na mapenzi hata kama hayatokaribia mapenzi ya mama kama wasanii wanavyosema "*wenye machozi karibu nao wakusaidie*" mapenzi ambayo ni ya mtu na jamii ambao husaidiana katika furaha na hudhuni.

Nyimbo nyengine ambayo wasanii wameonesha mapenzi ni wimbo wa (mama) wasanii wanasema kupitia wimbo huo:

Mama aliponivyaa halinyona mbaya,

Kanka chakula chema na nguo njema kuvwaa,

Kasoro kitu kimoji kaniti mwana hizaya,

Katika dondoo hili msanii anaonesha mapenzi kwa kumtumia mtoto juu ya kumsifu mama yake ya kwamba alipomzaa hakumuona na tatizo lolote, kwani aliweza kupewa mahitaji ya aina zote ambayo alihitaji mtoto kwa mzazi wake, kama chakula na nguo. Hata hivyo, wasanii wanatuonesha mapungufu ya kwamba wazazi wengi wanakiuka mila na desturi za jamii katika kanuni za dini zao kwa kuzaa watoto wa nje ya ndoa, jambo ambalo watoto wengi linawatia hudhuni kama ambavyo katika wimbo uliotangulia mtoto anaonesha kuwa alipatiwa mahitaji yote ya lazima kutoka kwa mama yake na anaonesha kasoro kwa mama yake ambae amemzaa bila ya baba, kitendo ambacho kinawahudhunisha watoto wengi wa aina hiyo na kuwakosesha haki zao za msingi kutoka kwa baba zao. Kwa mujibu wa mawazo ya Mulokozi (ameshatajwa) wimbo huu umeenda sambamba na hali halisi ya nyimbo bembelezi za watoto kutoka Makunduchi ambapo zimebeba maudhui mazito kumhusu mwanamke.

4.1.3 Mapenzi ya Uongo (Usaliti)

Kwa upande mwengine wasanii wa kazi za fasihi wanaelimisha jamii kwa kuonesha mapenzi ya uongo, kitendo hiki kinawahudhunisha na kuwaathiri wale ambao wana mapenzi ya udhati kwa wapenzi wao. Mlama katika tamthilia yake ya Hatia (1975) anaonesha mapenzi ya udanganyifu kwa kumtumia mhusika Juma ambae anaonesha kumpenda Cheja na kufanikiwa kumpa ujauzito na baada ya kuuelezwa jambo hili na Cheja, Juma anamkataa Cheja na kuukataa ujauzito huo na kumtaka Cheja amsingizie Sembule jambo ambalo linapelekea kuzuka kwa mgogoro wa familia za pande mbili. Mapenzi ya udanganyifu yako katika sehemu mbili; kwa upande wa

mwanamke kwa kumsaliti mwanamme, na mwanamme kumsaliti mwanamke. Katika nyimbo bembelezi za watoto, wasanii wameisawiri hali hii kwa kutuonesha kama watu wamo ndani ya ndoa lakini hutoka nje ya ndoa zao kwa kuwa na wapenzi wengine jambo hili husababisha kuvunjika kwa ndoa, au mtu aliesalitiwa na yeye huamua kutafuta mpenzi mwengine ili amkomoe mwenziwe. Kama wimbo unavyosema:

Kile kidau kijacho haikosi mna change,

Mna mkufu nitunge kadiri ya shingo yangu,

Siuvai siutupi wala simki mwenzangu,

Chamka mama mvyazi msiri wa mambo yangu,

Bwana wewe sikwebu waninyezeza nini kwangu.

Katika dondoo hilo lililodondolewa hapo juu linaonyesha wazi kuwa mwimbaji alikuwa ni mtu mwenye ndoa yake. Lakini hakuridhika kutokana na ndoa hio ingawa alikuwa anapata mahitaji yake. Wasanii wanaionesha dhamiri hii kwa kuwaasa wanandoa kubakia na waume zao katika ndoa. Haya yanadhihirika kwa kupitia mistari ufuatao wasanii wanasema*; kile kidau kijacho haikosi mna changu, mna mkufu nitunge kadiri ya shingo yangu, siuvai siutupi wala sinamka mwenzangu*. Neno mkufu limetumika kisitiari likiwa na maana ya kuwa ni mwanamme, mwanamme ambae ni mume wa nje ya ndoa. Mwanamke ambae yumo ndani ya ndoa hapendi wala hataki kumuona mwanamme huyu kuwa na mahusiano na mwanamke mwengine jambo ambalo haliwezi kuepukika kwa mwanamme asiye kuwa na ndoa. Waimbaji wanasema kuwa: *siuvai siutupi wala simki mwenzangu.* Maneno haya yanaonesha kuwa mwanamke hawezi kuolewa na waume wawili, hivyo basi ana hiyari kuikiuka ndoa yake na kwenda kwa mwanamme wa nje, ili

mwanamme huyo asiwe na mwanamke zaidi yake. Kwa upande wa mwanamke huyu anaona bora siri ampe mama yake kuliko kumpa mtu mwengine yoyote ambae anaweza kujua mahusiano waliyonayo na mwanamme huyo na hatimae kuvunjika kwa mahusiano hayo yasiyokubalika kijamii na kidini kama wanavyosema waimbaji wa nyimbo bembelezi; *chamka mama mzazi msiri wa mambo yangu*. Mtoto wa kike msiri wake mkubwa ni mama katika mambo yote ya kijamii, kiutamaduni na hata kiuchumi. Kupata na kukosa katika maisha ni jambo la kawaida hivyo haipendezi kuona mtu anajiingiza katika tabia zisizopendeza miongoni mwa tabia hizo ni kutokuwa mwaminifu na kuwa tamaa kwa kufanya usaliti (Sengo, 2009).

4.1.4 Malezi

Dhamira ya malezi pia ni miongoni mwa dhamira zilizojitokeza katika nyimbo bembelezi za watoto. Malezi ni uangalizi wa karibu wa wazazi kwa mtoto wao kiroho, kiafya, kiakili na kitabia: (www.ackyshine.com).

Kazi nyingi za fasihi ya Kiswahili zimeonesha umuhimu wa malezi ya wazazi kwa watoto wao, malezi haya yanapopatikana watoto wanakuwa katika misingi mizuri na yanapokosekana watoto wanaishia katika tabia mbaya kama vile wizi, uuzaji wa madawa ya kulevya, ujambazi n.k. Mwandishi wa riwaya ya watoto wa Mama Ntilie ameonesha dhamira hii kwa kuwaonesha wahusika kama vile, Kurwa, Peter na Zita kwa kupata malezi bora na vile vile mwandishi amewaonesha wahusika kama vile Dan na Doto kwa kukosa malezi bora kwa kuishia na kifo wakati walipojaribu kufanya ujambazi.

Msanii anawataka wazazi wawe na malezi sawa kwa watoto, ikiwa ni watoto wako au watoto wa mwenzako, tusibague wala kupendelea katika huduma zote tutakazowapa. Msanii anahimiza uwepo wa usawa katika malezi yao, kwani huenda yule atakaempenda akawa sie mwema kwako na yule unaemchukia akawa ndie mwenye kukufaa. Katika kulionesha hili wasanii wanasema kupitia wimbo bembelezi usemao; Mwana Mwema

Ukilea mwana mwema na mwana mui pia mlee,

Mwema ukimka chenga na mui mke chelele,

Humwiji akufaaye akukae maji mbeleee,

Katika wimbo wa mama mwema msanii ameonesha umuhimu wa malezi na kutofanya ubaguzi juu ya watoto hao, kwani huwezi kujua mtoto gani atakae kufaa utakapofikwa na shida pamoja na matatizo. Watu wengi wanategemea watoto wao wanapokuwa watu wazima ili waweze kuwasaidia na kuwatunza. Hivyo basi, si vyema kuonesha ubaguzi katika malezi, kwani baadhi ya watu hubagua hata kama watoto wao wenyewe kitendo ambacho kinaleta chuki miongoni mwa watoto wenyewe. Wimbo mwengine ambao mwandishi ameonesha dhamira ya malezi ni wimbo uitwao Mama kwa kusema;

Mama aliponivyaa halinyona mbayaaa,

Kanka chakula chema na nguo njema kuvwaaa,

Kasoro kitu kimoja kanyiti mwana hizaya,

Katika wimbo uliyodondolewa hapo juu inaonesha umuhimu wa malezi ya mama kwa mtoto wake, kwani ni jukumu kati ya wazazi wawili kuhudumia watoto wao. Wimbo unaonesha kuwa mtoto huyu ni wa upande mmoja ambae hakuwa na baba, bali jukumu lote la malezi lilisimama kwa mama ambaye alijikubalisha kwa kila kitu.

Hata hivyo, mtoto anatoa masikitiko yake juu ya kuwa ni mtoto wa nje ya ndoa lakini nae alikuwa na mapenzi makubwa kwa mama yake pale aliposema: *Mama aliponivyaa halinyona mbayaaa, Kanka chakula chema na nguo njema kuvwaaa.* Wasawahili husema “nani kama mama” maneno yanathibitisha upendo na mapenzi makubwa ya mtoto kwa mama yake kama alivyosema Shaaban Robert ndani ya kitabu chake cha Mapenzi Bora. Wimbo huu pia unadhihirisha kwamba mama alikuwa na mapenzi na malezi mazuri juu ya mtoto wake kwa kumtimizia mahitaji yote yanayostahiki kwa kumpa chakula, mavazi na malazi, kwani tumeshuhudia watoto kadhaa wakitupwa majaani na sehemu nyengine kwa kukosa huduma muhimu na malezi bora. Penye huba, pana huruma na huduma (Sengo, 2014).

4.1.5 Nafasi ya Mwanamke

Mwanamke katika riwaya huchorwa kulingana na nafasi yake katika jamii ambapo huonekana kama ni chombo cha kumstarehesha mwanamme, kiumbe dhaifu na tegemezi Kiango (1992). Mbali na riwaya, kazi nyingi za fasihi ya Kiswahili zimemchora mwanamke katika mitazamo mbali mbali kama vile mwanamke kama mama, mwanamke kama pambo, mwanamke ni mtu asie na maamuzi, mwanamke ni mtu mwenye tamaa n.k.

Kupitia nyimbo bembelezi za watoto wasanii wameonekana kumchora mwanamke kwa namna tofauti kulingana na namna anavyojitokeza, anavyochukuliwa na kuonekana katika jamii.

4.1.6 Mwanamke ni Mtu Asie na Maamuzi

Dhamira hii ni miongoni mwa dhamira maarufu zinazopatikana katika fasihi. Dhamira hii imekuwa ikiwasilishwa kwa namna mbalimbali kulingana na

madhumuni ya kila mwandishi au msanii anapowasilisha kazi yake ya kifasihi kwa jamii. Dhamira hii pia imedhihirishwa katika nyimbo bembelezi za watoto zinazotumiwa kutoka Makunduchi kwa kusema kupitia wimbo wa Dume kongwe:

Baba na mama watende kunioza dume kongweee,

Halisafiri halyende kazi kupiga matongeee,

Likikaa mvunguni hunguruma kama gombeee.

Katika dondoo hili wasanii wanaonesha kuwa mwanamke aliyeoneshwa katika wimbo huu, hakuwa na maamuzi katika kuyakabili maisha yake ya ndoa na hakupewa uhuru wa kumchagua ampendae jambo ambalo linampelekea aoneshe masikitiko yake kwa kusema; *baba na mama watende kunioza dume kongwe*. Neno "watende" limetumika kuonesha kulazimishwa mwanamke huyo kuingizwa katika ndoa pasi na yeye mwenyewe kushauriwa jambo ambalo linakiuka haki za binadamu kwani mwanadamu anatakiwa awe huru na awe na maamuzi yake katika kuamua mambo yake. Wasanii wameisawiri dhamira hii katika kuonesha hali halisi waliyonayo wanawake katika jamii nyingi za kiafrika kitendo ambacho kinakwenda kinyume na maamrisho ya dini na kanuni za nchi ambazo zinamtaka mwanamke apewe uhuru na uamuzi wa kuchagua.

Farsy (1956) anaeleza kwamba ndoa inapofungishwa lazima wapatikane mashahidi na idhini ya bi harusi na idhini ya walii wake yaani baba yake; kama hana baba jamaa yake aliyekuwa karibu nae zaidi kuliko wengine, kama hana ipatikane idhini ya mfalme, raisi au kadhi. Rwezaura (1981) katika kuelezea sheria ya ndoa ya kiislamu ya mwaka (1971) anasema sheria inampa uwezo kadhi wa dini ya kumfungisha ndoa kufuata madhehebu ya dini ya Kiislamu. Leseni hii hutolewa na msajili mkuu chini ya kifungu cha 30 (4). Kadhi wa dini ya Kiislamu anaweza

kuteuliwa kuwa msajili wa ndoa kutokana na sheria ya ndoa. Hivyo basi, wasanii katika kuonesha masikitiko na hudhuni wanazozipata wanawake hao wanafikia hatua ya kuwafananisha waume zao na dume kongwe ambalo limeishiwa na kila kitu. Hayo yote yanatokezea pasi na ridhaa za wanawake na kutoshirikishwa katika maaamuzi ya mume wanaemridhia,wazee wanafanya hayo kwa kuona kuwa mtoto wa kike si mtu wa kushauriwa ni mtu wa kuamuliwa tu kama wimbo unavyoeleza. Mlacha (1996) anaeleza kwamba, ndoa ni makubaliano baina ya mwanamke na mwanamme, kwamba wapo tayari kuishi pamoja na kuanzisha familia ambapo mtu mmoja atakuwa mama na mwengine atakuwa baba katika familia hiyo iliyoanzishwa (Omari, 2014). Kutokana na umuhimu wa ndoa kama ilivyoonekana katika jamii baadhi ya watoto wa kike huozwa wakiwa wadogo tu, pasi na ridhaa zao maadamu wazazi wamekwisha kuamua mtoto hawezi kupinga hata kama hajaridhia kitendo hicho, hali iliyopelekea kuibuka wimbo bembelezi usemao Dume Kongwe kwa kusema: *“baba na mama watende kunioza dume kongwe”*.

Dondoo lililoonesha kwamba mtoto mwanamke hapa ameozwa kwa mwanamme asiye chaguo lake kwa kulazimishwa na wazee wake. Kwa wataalamu na watafiti wa masuala ya kijamii na kijinsia, hukiona kitendo hiki kama ni ukatili wa kijinsia kwa kuwa kinamkosesha mtoto wa kike haki zake na uamuzi wake mwenyewe katika maisha (Ngaiza, 2002) amenukuliwa na (Omar, 2014).

4.1.7 Mwanamke ni Mtu Mwenye Tamaa

Dhamira hii imesawiriwa katika nyimbo bembelezi kama inavyosawiriwa katika kazi nyengine za fasihi, waandishi na wasanii wanaionesha dhamira ya wanawake wenye tamaa ili waweze kujiepusha nayo kwani tamaa haina mwisho mwema. Katika

wimbo wa kidau wasanii wamemuonesha mwanamke kwa kufanya tamaa ya kumpenda mwanamme mwengine wa nje ya ndoa na kumuacha mumewe wa ndoa kwa kumwambia kuwa hamtaki ya nini kumfata fata. Haya yanadhihirika kupitia wimbo wa Kidau usemao:

Kile kidau kijacho haikosi mna changu,
Mna mkufu nitunge kadiri ya shingo yangu,
Siuvai siutupi wala simki mwenzangu,
Chamka mama yangu msiri wa mambo yangu,
Bwana wewe sikwebu waninyezeza nini kwangu.

Katika dondoo iliyodondolewa hapo juu wasanii wanatuonesha kuwa wanawake wamekuwa na tamaa pamoja na kuwaacha waume zao wa ndoa kwa kufuata wanaume wa nje. Katika wimbo uliotangulia mwandishi anasema kuwa: *kile kidau kijacho hamkosi mna changu, mna mkufu nitunge kadiri ya shingo yangu.* Hapo msanii anaonesha tamaa ya mwanamke kumpenda mwanamme wa nje ya ndoa kwa mapenzi, jambo ambalo linapeleka kuiathiri familia na kuongezeka kwa talaka katika jamii. Wanawake wenye tamaa mara nyingi husababisha kuvunjika kwa ndoa zao pia huleta madhara katika familia, kama vile maradhi yanayopatikana kwa njia za udanganyifu. Hata hivyo, wasanii wanaonesha msimamo wa mwanamke katika kumkataa mwanamme wazi wazi kwa kusema; *bwana wewe sikwebu waninyezeza nini kwangu*.

Wimbo unaonesha kuwa mwanamke anamkataa mumewe wa ndoa kwa tamaa ya mapenzi ya mwanamme wa nje.

4.1.8 Elimu

Elimu ni kitu muhimu kwa watoto kama taifa linataka kuendelea. Hata hivyo katika nchi zinazoendelea kama Tanzania suala la elimu bado halipewi umuhimu unaostahili, watoto kutoka katika familia masikini bado hawana uhakika wa kupata elimu, licha ya porojo za viongozi wa kisiasa kwamba hakuna mtoto atakaeshindwa kusoma kwa sababu ya umasikini (Nyangwine na wenziwe 2004 – 2007). Sengo na Kiango (2011) wanasema katika nchi zetu wajibu wa elimu, wasomi ni mkubwa mno. Kwani wao ndio wanaotegemewa kufanya utafiti juu ya matatizo tuliyonayo, kuyaelewa na kuwashirikisha watu ili tupate kuyatatua. Jilala (2016) anasema kuwa elimu ni suala mabalo limejadiliwa katika riwaya ya Rosa Mistika katika dhana ya uhasi, anaendelela kusema kuwa mwandishi anaonesha kuwa elimu ndio chanzo cha mgogoro baina ya wazazi na watoto wao. Vile vile ametumia riwaya ya Tata za Asumini kuwa elimu imetumika katika njia hasi na imekuwa ni chanzo cha migogoro katika jamii, kwani mhusika Asumini alibadilika baada ya kufika Chuo Kikuu na kuacha mafunzo aliyofunzwa na wazazi wake. Hivyo katika nyimbo bembelezi wasanii wameonesha dhamira hii kwa mawanda mapana, katika wimbo wa Mtoto wangu mzuri inaonesha umuhimu wa elimu kwani wazazi wanatoa hamasa kwa watoto wao ili wapende kusoma kwa kusema:

Ooooh mtoto ooooh mtoto,

Mtoto wangu mzuri iiii,

Chamveleka skuli iiii,

Mtoto wangu mbaya aaaa,

Chamveleka Ulaya aaa,

Ooooh mtoto oooh.

Katika dondoo lililodondolewa hapo juu linaonesha umuhimu na faida ya elimu kwani mzazi anawatia hamasa watoto wake kwa kuwaambia yule ambae ni mzuri atampeleka skuli. Kwani mara nyingi elimu inapatikana katika sehemu maalum kama vile maskulini na vyuoni. Hivyo basi, mzazi anawataka watoto wake wote wapate elimu ili iweze kuwasaidia maishani mwao, kwani tunaamini kuwa elimu ni mkombozi wa maisha katika watu wa rika zote. Pia mzazi anatuonesha kwa yule mtoto atakaekuwa mbaya asiye fuata sheria na maelekezo kutoka kwa wazazi wake atampeleka mbali na nyumbani, katika wimbo huu wasanii wametumia neno "Ulaya" likiwa na maana kuwa ni sehemu mbaya ambayo watoto hawatopata maendeleo. Katika kujua umuhimu wa dhamira hii mtafiti aliwauliza maswali watafitiwa kwa kusema "Jambo gani lililowasukuma wazee na kuwapelekea kuwaimbia watoto wao wimbo huu?" mzee mmoja alianza kujibu kwa kusema:

Suwe wazee twevu tunapendelea sana kwa wanakele wavate elimu ya sukuli na chuoni ili iweze kuwasaidia katika maisha yao, wakifanikiwa wanakele na suwe wazee tuchafwaidika javivo. Twevu tunawaimbia wanakele ili wavitambue kwamba sukuli ni sehemu nzuli na pia wawe wanapendelea kwenda sukuli. Katika enzi zetu nchi za Ulaya twevu tunakona hakunafwaa kwenda wanakele wema hivyo twevu tukawaimbia kwa kuwatisha ili wawe wanakele wazuli.

Kiswahili sanifu

Sisi wazee tulikuwa tunapenda sana kwa watoto wetu wapate elimu ya shule na chuoni ili iweze kuwasaidia katika maisha yao, wakifanikiwa watoto na sisi wazee tutafaidika hivyo hivyo. Tulikuwa tunawaimbia watoto ili wajue kwamba shule ni sehemu nzuri na pia wawe wanapendelea kwenda shule. Katika enzi zetu nchi za

Ulaya tulikuwa tunaona hakufai kwenda watoto wema hivyo tulikuwa tukiwaimbia kwa kuwatisha ili wawe watoto wazuri.

Kutokana na maelezo ya mtafitiwa huyu inaonesha wazi kuwa wazee wa zamani walikuwa na imani kwamba skuli ni sehemu ya kuwaletea watoto maendeleo, na Ulaya ni sehemu iliyokuwa mbaya na haifai watu kuenda huko, hii ina maana kuwa hulka, mila, desturi na tabia za watu zinatafautiana kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine na kutoka bara moja kwenda bara jengine. Hivyo basi, waliona ni vyema kuwaimbia watoto wao nyimbo hizo ili kuwaonya wasipende maisha ya Ulaya.

Katika kuonesha kuwa elimu ni muhimu (Nyerere, 1962), mara tu baada ya kupatikana uhuru wa Tanganyika, alitangaza kwamba katika jamii yetu kulikuwa na maadui watatu ambao ni maradhi, ujinga na umasikini. Hata hivyo aliongeza kwamba, ujinga ndio adui mkubwa kuliko maadui hao wengine wawili na kwamba adui huyu alihitaji kushughulikiwa mara moja ili jamii inusurike na maradhi na umasikini (Omari, 2014).

Vile vile wasanii wanazidi kutuonesha umuhimu wa elimu na kwamba elimu haina mwisho. Mtu yoyote asiwe mwenye kukata tamaa na elimu na wala asiigawe elimu katika makundi mawili; elimu ya dunia na elimu ya akhera. Elimu yoyote kwa mwenye kujifunza inamletea manufaa, kama wasanii wanavyosema katika wimbo wa Msikiti wa jibondo usemao:

Msikiti wa jibondo kandili mbili zawakaa,

Wamo wasomaji vyuo na waandikao nyarakaa,

Nyama zote nzili kasoro kia lya pakaa,

Katika dondoo lililodondolewa hapo juu inaonesha wazi kuwa elimu zote ni muhimu katika maisha ya mwanadamu. Wasanii wanasema katika mstari wa mwanzo "*msikiti wa jibondo kandili mbili zawaka*" katika msikiti ni sehemu ya kufanyia ibada lakini wasanii wanatwambia kuna kandili mbili zawaka, kandili hizi zimesimama kama ni elimu na ni muangaza wa kuwatoa watu gizani. Kwani elimu inawatoa watu kizani na kuwapeleka kwenye nuru kwa hiyo wasanii wametumia neno kandili kisitiari likiwa na maana ya elimu yenye manufaa. Katika kuonesha hakuna matapo kwa upande wa elimu wasanii wanasema: *wamo wasomaji vyuo na waandikao nyaraka.* Katika mstari huu wasanii wameonesha msikiti kama ni sehemu na chanzo kikuu cha kupatia elimu. Msikiti umesimama kuwakilisha skuli, chuo, maktaba au chuo kikuu ambazo ni sehemu kuu zinazotolewa elimu na ni sehemu za kuhifadhia vitabu na nyaraka mbalimbali ambazo zimetungwa na watu na hufanyiwa kazi. Hata hivyo, wasanii wanaonesha kwamba soma kadri ya uwezo wako lakini elimu hutoifikia mwisho wake kwa kusema "*nyama zote nzili kasoro kia lya paka".*

Kwa mujibu wa misingi ya nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inampa msomaji uhuru wa kusoma, kuielewa na kuihakiki kazi ya fasihi, mtafiti ameweza kuzisoma na kuzielewa nyimbo za kubembelezea watoto na kutoa dhamira, ujumbe na mafunzo yapatikanayo katika nyimbo hizo. Usomaji makini ndio uliomuezesha mtafiti katika kuzibainisha na kuzichambua dhamira zilizojitokeza katika nyimbo bembelezi (Iser, 1974 na Fish, 1980).

4.1.9 Utamaduni

Kwa mujibu wa chapisho la sera ya utamaduni Tanzania la mwaka 1997, utamaduni ni jumla ya mambo yote yanayobuniwa na jamii ili kukidhi utashi na maendeleo yake, ni mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wao wa mambo, na taratibu zao

zote za kuendesha maisha zinazowatafautisha wao na jamii nyengine. Aidha sera hiyo inabainisha nguzo za utamaduni kuwa ni mila na desturi, lugha, sanaa, michezo na historia ya jamii. Wamitila (2003) anasema utamaduni ni dhana pana, ni uzoefu wa kimaisha wa watu. Ramadhan (2013) anaeleza kwamba utamaduni ni mfumo au utaratibu wa maisha mbao jamii inaufuata katika maisha yake ya kila siku ikijumuisha mila, desturi, miiko, matambiko, jando na unyago. Utamaduni wa jamii ndio hutoa dira na mwelekeo wa mambo mbalimbali katika jamii yanapaswa kuendeshwa na wanajamii ili kuleta uhusiano mzuri miongoni mwa watu, upendo, kuheshimiana na kushirikiana katika jamii. Jilala (2016) anasema utamaduni ni uzoefu wa kimaisha watu wa jamii ambao hutumia lugha moja kama njia ya mawasiliano. Jilala (ameshatajwa) anaendelea kusema kuwa kila jamii ina utamaduni wake ambao ni tofauti na ule wa jamii nyengine, na tofauti hii huleta tofauti katika utambuzi na uelewa wa malimwengu. Hivyo basi, utamaduni ni mkusanyiko wa michakato ya kijamii ambayo huiwezesha jamii hiyo kujieleza na kujitambulisha pamoja na kufanya shughuli za kila siku. Utamaduni wa jamii ni kitu kizuri ambacho kinahitaji kufuatiliwa na kusimamiwa ili kuhakikisha kwamba utamaduni unatoa mchango mkubwa katika kuliletea taifa maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Kazi nyingi za fasihi zimetumika katika kuutambulisha utamaduni katika sehemu mbalimbali mfano mwandishi Shafi katika riwaya ya Kuli amemuonesha bi Mashavu kwa kusema “ingawa chumba kilikuwa kidogo, bi Mashavu alikiweka katika hali ya usafi kabisa, kitanda cha samadari kilichokuwemo humo kilitandikwa vizuri shuka nyeupe iliyofumwa kwa maua mekundu katikati”. Hivyo basi, nyimbo bembelezi za watoto kutoka Makunduchi zimekuwa chachu kubwa za kuutambulisha utamaduni

wa Kizanzibar na hususani utamaduni wa Kisiwa cha Unguja wasanii wanasema katika wimbo wa kijaluba kwa kusema:

Nyevu nyende matembezi upande wa Bungi Pwani,

Nikakuta kijaluba kina karafuu kati,

Kijaluba hali ino mwenyewe yu hali gani?

Katika dondoo lililotangulia hapo juu linatuonesha utamaduni wa watu katika jamii moja ya kutembeleana kwa uzima na ugonjwa, kitendo hiki kinawapa faraja na upendo kwa wale wenye kutembeleana. Utamaduni mwengine unaojitokeza katika wimbo huu ni utamaduni wa usafi na urembo kwa kutumia malighafi ya asili nayo ni karafuu kama wanavyosema wasanii "*nikakuta kijaluba kina karafuu kati, kijaluba hali ino mwenyewe yu hali gani?"*

Kutokana na wimbo huu mtafiti alimuuliza mtafitiwa mmoja kijaluba kina maana gani hata ifike hatua ya kutumiwa katika nyimbo za kubembelezea watoto? Mtafitiwa alianza kujibu kwa kusema:

"Kijaluba ni kifaa au chombo kinachotumiwa kwa ajili ya kutulia manukato chumbani. Kwa zamani kifaa kino chevu kinatulwa mezani, kutokana na maendeleo ya watu vino sasa kijaluba kino kinatulwa juu ya diresing".Dhumuni kubwa la kino kijaluba ni nktuwa vitu vya kusugulia mwili kama javile liwa, karafuu, mawaridi, asumini, mipompia na mipachori. Vitu vyote vino kwa pamoja huwa ni unga unga uliochanganyishwa na kuleta harufu nzuri kwa mwenye kuisikia. Mtafitiwa huyu anaenelea kusema kuwa vino sasa nyumba chache sanakuchangia nani na ukakosa kuchona kijaluba ambacho kati hakina vitu javino.

“Kijaluba ni kifaa au chombo kinachotumiwa kwa ajili ya kuwekea manukato chumbani. Kwa zamani kifaa hiki kilikuwa kinawekwa mezani, kutokana na maendeleo yanayojitokeza kwa watu wa sasa kijaluba hiki huwekwa juu ya dressing”. Madhumuni makubwa ya kijaluba ni kuweka vifaa vya kusugulia mwili kama vile liwa, karafuu, mawardi, asumini, mipompia na mipachori. Vitu vyote hivyo kwa pamoja huwa ni unga uliochanganywa vizuri na kuleta harufu nzuri kwa kila mwenye kuisikia. Mtafitiwa huyu anaendelea kusema kuwa *ni nyumba chache sana za zamani utakazoingia ukakosa kukuta kijaluba ambacho hakina vifaa ndani yake.*

Kutokana na maelezo ya mtafitiwa huyu inaonesha wazi kuwa Wazanzibar wengi wanapenda kujipamba na kusafisha miili yao kwa kutumia vitu vya asili. (Sengo,2009) anaeleza kwamba kila jambo katika jamii lina dhima maalumu, kwa mfano, mwanamke kufanya kazi za nyumbani ni wajibu wake na kwamba msanii au mwandishi anapomsawiri mwanamke kutekeleza wajibu wake hamnyanyasi hata kidogo bali anamtendea haki, hivyo usawiri wa mwanamke katika wimbo huu na usafi wake kama kilivyo kijaluba ni sahihi na wala hauna shaka hata kidogo.

4.1.10 Ukweli

Theobald Mvungi (1995) amejenga dhamira ya ukweli bila woga. Hii inajionyesha katika shairi lake “*kazi yetu harakati*” anapomsifu mwandishi Mhando kwa kazi yake ya Lina ubani. Mwandishi Mhando kasema ukweli kuhusiana na walaji majahili bila ya kuwapaka mafuta kwa mgongo wa chupa. Hivyo ndivyo inavyostahili kwa msanii alie makini. Kwa kusema:

Ameweka dawa kali kidonda kipate hali,

Mhando kasema kweli ile kweli ilo kali,

Kwa walaji majahili dawa yao ni ukali,

Kwa kiziwi aelewe ni vitendo umwonyeshe.

Kutokana na maelezo haya inaonesha wazi kuwa wananchi wanakerwa na matendo yanayofanywa na wale waliopewa nafasi za kuongoza watu. Hali hii pia imedhihirika katika nyimbo bembelezi za watoto baada ya wasanii kuonesha hisia zao za ukweli kwa yale waliyofanyiwa na wazazi wao. Dhamira hii imejitokeza katika wimbo wa Dume kongwe na Kidau kwa kusema:

Baba na mama watende kunioza dume kongweee,

Halisafiri halyende kazi kupiga matongeee,

Likikaa mvunguni hunguruma kama gombeee.

Katika dondoo hili wasanii wanaonesha ukweli kupitia kwa wanandoa. Vijana wa zamani walikuwa hawana fursa ya kuchagua wapenzi wawapendao, maamuzi yote yanaamuliwa na wazee na watoto hawawezi kupinga kwa yale waliyoamuliwa. Vijana wa kike na wakiume walikuwa wanaozeshwa kwa amri za wazazi wao pasi na kupewa uhuru wa kuchagua, jambo hili lilipelekea wanandoa wengi kuingia katika ndoa ambazo hawakuziridhia kama ambavyo wasanii wanavyosema katika mstari wa mwanzo wa wimbo huu; "*Baba na mama watende kunioza dume Kongweee"*. Maneno haya yanaonesha wazi kuwa hapakuwa na maridhiano baina ya wawili hawa, kwani mwanamke anaamua kuonesha masikitiko na dukuduku lake kwa kupitia nyimbo bembelezi. Hali hii vile vile imejidhihirisha kupitia wimbo wa Kidau pale wasanii waliposema *bwana wewe sikwebu waninyezeza kwani?* Katika mstari huu pia inaonesha ukweli wa mwanamke kuwa ni mtu mwenye msimamo na hatakiwi kuyumbishwa katika maisha, anatoa maamuzi ya kumkataa mume kwa kumpa ukweli kama alivyosema: "bwana wewe sikwebu waninyezeza nini kwangu?" Finnegan (1970) alieleza kwamba mayaya walikuwa wakitumia nyimbo bembelezi

katika kutoa hisia zao kutokana na dhulma wanazotendewa na matajiri wao, ambapo katika wimbo tuliouchambua tumeona namna mwanamke alivyozungumza ukweli na kutoa hisia zake kwa dhulma aliyotendewa ya kuozwa Dume kongwe.

4.1.11 Siasa

Katika kazi nyingi za fasihi siasa imezungumziwa kwa njia pana, siasa imezungumziwa katika suala la ukombozi kwa kuweza kujikomboa kutoka katika utawala wa kikoloni (Mhilu na wenzake, 2008). Katika kuibua dhamira hii wasanii wameonesha ukombozi wa kisiasa dhidi ya unyonyaji, uonevu na ukandamizaji wa aina zote. Hivyo basi, wasanii wa nyimbo bembelezi wameitumia dhamira ya kisiasa katika kusawiri hali halisi iliyokuwepo katika kipindi cha ukoloni kama inavyosawiriwa katika kazi nyengine za fasihi. Wimbo bembelezi wa kidau unaonesha hali hiyo kama usemavyo**;**

Kile kidau kijacho nnageza mna changu,
Mna mkufu nitunge kadiri ya shingo yangu,
Siuvai siutupi wala simkii mwenzangu,
Chamka mama mzazi msiri wa mambo yangu,
Bwana wewe sikwebu waninyezeza nini kwangu?

Katika dondoo lililodondolewa hapo juu tumeona namna wasanii walivyoona ndoto za kupata uhuru “kidau” kimefananishwa na uhuru, uhuru ambao ulitolewa na wakoloni waliokuwa wakitawala Zanzibar (1963). Uhuru huu uliopatikana ulikuwa ni wa bandia ambao ulifikia mikononi mwa watawala wengine wa kiarabu na kuwaacha wananchi wakiwa katika mateso ya kutumwa na kutawaliwa, na Waarabu ambao walikuwepo Zanzibar, katika mstari usemao “*siutupi siuvai wala simki*

mwenzangu” maneno haya yanaonesha kwamba Wazanzibar walikwisha choka kutawaliwa hivyo waliona waanzishe mapambano kimya kimya na baada ya kufanikiwa, wameamua kuunganisha nchi yao na Tanzania bara ambao wanaifananisha nchi hiyo na mama kama wanavyosema “*chamka mama mzazi atunzae siri zangu*”. Tanzania bara hapa imehusishwa na mama mzazi, kwani ni nchi ya karibu ambayo haitokuwa rahisi kuchangia maadui watakaoweza kuihujumu Zanzibar. Katika kumalizia wimbo huu wasanii wanasema “*bwana wewe sikutaki waninyezeza nini kwangu?*” Maneno haya ni mapinduzi yaliofanywa Zanzibar baada ya Wazanzibar kuchoka kunyanyaswa, kunyonywa, kutawaliwa na kufanywa watumwa katika nchi yao. Hivyo, wimbo huu ulikuwa unaelezea namna Zanzibar ilivyofanikiwa kupata uhuru na baada ya kupata uhuru huo, bila hata ya kufikiri wakaamua kujiunga na Muungano na Tanganyika ili kupata hifadhi dhidi ya maadui, lakini pia waafrika waliopata uhuru wanapaswa kuwakumbuka Waafrika ambao hawajapata uhuru kwa kusaidia kwa hali na mali nao wapate uhuru wao (Nyerere, 1973) akinukuliwa na (Omari,2015).

4.1.12 Uchumi

Kazi nyingi za kifasihi huzungumzia dhamira hii katika hali halisi ya kijamii, wasanii wa nyimbo bembelezi nao wameielezea dhamira ya uchumi kwa jinsi walivyojaaliwa, wameeleza namna nchi ya Zanzibar ilivyo na utajiri kutokana na rasilimali zake ziliomo katika nchi, miongoni mwa raslimali hizo ni karafuu ambazo zinaingiza pato kubwa na kuingiza pesa za kigeni kwani karafuu ndizo zao kuu la Zanzibar katika kuingiza pesa za kigeni, mtafitiwa alieleza hayo katika wimbo wa Bungi pwani kwa kusema;

Nyevu nende matembezi upande wa Bungi pwani

Nikakuta kijaluba kina karafuu kati

Kijaluba hali ino mwenyewe yu hali gani?

Ooooh mtoto ooooh

Katika dondoo hili lililotangulia hapo juu wasanii wameonesha “kijaluba” kikiwa na maana ya nchi ambayo imejaa uzuri wa neema na utajiri wake namna kwa namna, kwani wameonesha katika upande mmoja wa kisiwa na Zanzibar ni mchanganyiko wa visiwa viwili Unguja na Pemba wameeleza kuwa ni sehemu moja tu waliyokwenda kimatembezi na ile raslimali waliyoikuta. Maendeleo ya nchi yanategemea ukuaji wa kiuchumi, nchi ni lazima iwe na rasilimali yake ili iweze kuzalisha na kununua vifaa na mahitaji mengine ambayo hayawezi kupatikana katika nchi husika. Uchumi ukikuwa katika nchi matabaka hutoweka kwani mahitaji ya lazima kwa jamii yanatekelezeka kama makazi bora, mavazi na chakula, pia huduma kama vile elimu, afya na huduma za kijamii zinapatikana pasi na kuyumba kwa nchi. Chuki na uhasama baina ya viongozi na wananchi zinapungua kwani ahadi zinazotolewa na viongozi zinatekelezwa ipasavyo kwa wakati.

4.2 Mbinu za Kisanaa Zilizojitokeza katika Nyimbo Zilizoteuliwa

Katika sehemu hii mtafiti amebainisha na kuchambua data zinazolenga kukamilisha lengo mahsusi la pili ambalo limehusu kubainisha mbinu za kisanaa zinazotumiwa na wasanii katika kusawiri dhamira zinazojitokeza katika nyimbo bembelezi za watoto. Kazi yoyote ya fasihi ili ivutie iwe imepambwa ua kuundwa kwa kutumia vipengele mbalimbali vya kisanaa kwa kuifanya kazi hiyo iwe ya kisanaa. Senkoro (1988 na 2011) anasema matumizi ya lugha ni moja wapo ya mbinu za kisanaa zinazotumiwa na watunzi kwa kazi mbalimbali za fasihi zikiwemo nyimbo katika kusawiri dhamira katika kazi zao. Matumizi haya ya lugha katika kazi za fasihi zikiwemo nyimbo ndio

yanayowafanya watu kupenda au kutokupenda kazi za wasanii, msomaji anaweza kuvutiwa na kazi ya fasihi ambayo imepambwa pamoja na kutumiwa vipengele mbalimbali vya mbinu za kisanaa. Vile vile msomaji anaweza akachukizwa kusoma au kuangalia kazi za fasihi ambazo watunzi wake hawakutumia mbinu za kisanaa. Hivyo basi, wasanii wa nyimbo bembelezi za watoto kutoka Makunduchi wametumia kipengele cha mbinu za kisanaa kwa mawanda mapana, miongoni mwa mbinu hizo ni kama vile sitiari, ishara, takriri, usimulizi, taswira, nahau, tashhisi, tashbiha, mbinu ya kuuliza maswali na nyenginezo.

4.2.1 Sitiari

Mulokozi na Kahigi (1979) wanasema kuwa sitiari ni uhamishaji wa maana na hisi kutoka katika kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyengine, vitu hivyo vinavyohusishwa kwa kawaida huwa havina uhusiano wa moja kwa moja. Gibbe (1990) anasema sitiari ni semi ambayo hulinganisha vitu viwili mlinganisho huu hufanywa kwa kudokezwa tu. Kwa mujibu wa Mulokozi na Kahigi (1979) wanasema dhana nyingi katika kazi za fasihi hazielezwi kwa uwazi, mbinu hii vile vile imejitokeza katika nyimbo bembelezi za watoto ambazo nazo hazijaelezwa kwa uwazi kwa kile ambacho kinakusudiwa. Lakini zimetumia mbinu hii kulinganisha vitu mbalimbali mfano katika wimbo wa “Kidau” mwandishi ametumia sitiari ya kidau na mkufu akiwa na maana mwanamme wa nje ya ndoa ambae amebeba zawadi ya kumpelekea mwanamke wake, na mwanamke huyo yupo tayari kumpokea mwanamme huyo na kumwacha mumewe wa ndoa kwa kumkataa.

Vile vile kwa upande mwengine maneno haya yametumika kisitiari kwa upande wa siasa “Kidau” imetoa maana ya uhuru, uhuru ambao haukuwafikia wananchi bali ulifika katika mikono ya watawala wengine wa kigeni na “Mkufu” ukiwa na maana

ya nchi ya Zanzibar. Pia sitiari nyengine imejitokeza katika wimbo mwana mwema neno kama vile “maji” limetumika kisitiari likiwa na maana manufaa na huduma ambazo mzee atazipata kupitia mtoto huyo atakapokuwa mtu mzima na mzee akiwa hana nguvu tena.

Nadharia ya Semiotiki imejengwa katika mihimili mitano ambayo ndiyo msingi mkuu katika kuzifumbua ishara katika kulionesha hili wasanii wametumia msingi wa ujumbe katika uwasilishaji wa kazi zao kwani katika nyimbo zote mtafiti alizozichunguza ujumbe unapatikana kwa kadri wa msanii alivyohitajia ufike kwa jamii lengwa. Katika wimbo wa Mwana mwema msanii ametumia sitiari ya maji ili kuweza kutoa ujumbe kwamba, usiwe na ubaguzi katika ulezi kwani atakae kusaidia katika maisha huwezi kumjua hivyo watoto wanaolelewa wanatakiwa kupewa haki sawa katika malezi yao.

4.2.2 Ishara

Ishara ni neno au usemi wenye maana inayowakilisha dhana nyengine kwa kuhusiana nayo. Yaani, neno au usemi huo huwa na viwango viwili vya maana. Katika fasihi dhana ya ishara inatumika kuelezea kitu fulani ambacho huwakilisha kitu chengine. Ishara inaweza kuwa na msingi wa kisitiari Jilala (2016). Senkoro (1982) anasema maneno kama vile taa, mwenge, hutumika kuwakilisha utambuzi, ujuzi, au inaweza kuwa na msingi wa kitaashira kama kaburi, jeneza, fuvu, ambayo hutumika kuwakilisha mauti. Katika nyimbo bembelezi wasanii wameonesha ishara mbalimbali katika kuibua dhamira tofauti zinazopatikana katika nyimbo hizo ishara zilizotumika ni kama vile “kandili mbili, wasomaji wa vyuo, nyaraka, nyama zote nimekula na kasoro kia la paka”. Ishara zote hizi zimejitokeza katika wimbo wa Msikiti wa jibondo zikiwa na maana tofauti kandili mbili zikiwa zinaashiria

mafanikio, nuru na mwangaza katika kutafuta elimu, wasomaji wa vyuo na nyaraka ishara hizi zikiwa na maana ya elimu inayopatikana katika nchi na haijabaguliwa aina gani ya elimu; kama elimu ya dini au dunia, “nyama zote nimekula” ishara hii inashiria kuwa wasanii wanaonesha ingwa utajitahidi kutafuta elimu ya kila aina lakini elimu hiyo hutoifikia mwisho na wala hutokuwa mjuzi wewe bali kuna wajuzi na wataalamu ambao wamekuzidi, “kasoro kia la paka” inaonesha kuwa elimu haina mwisho na wala hakuna atakaefikia kileleni.

Ishara nyengine ambazo zimejitokeza katika nyimbo bembelezi za watoto ni kama vile “kijaluba na karafuu” katika wimbo wa kijaluba. Neno “kijaluba” ikiwa na maana ya urembo, uzuri, usafi na tabia ya mtu, na neno “karafuu” ikiwa na maana ya zana za kusafishia mwili ambazo mara nyingi wazanzibar wanatumia wakichanganya na vitu vyengine. Kwa upande wa siasa neno “kijaluba” limetumika kama ishara ya nchi yenye neema na utajiri, na neno “karafuu” ni rasilimali na uchumi unaopatikana katika nchi. Ishara nyengine wasanii wameionesha katika kupitia wimbo wa Dume kongwe neno dume kongwe linaashiria mwanamme ambae amekwisha pitwa na wakati, amezeeka na hawezi kutekeleza haki za msingi zinazotakiwa katika ndoa. Mwanamke anaonesha hisia zake kwa lile jambo ambalo anategemea kufanyiwa na mumewe lakini linakosekana. Hivyo anawalaumu wazazi wake kwa kumkosesha uhuru na kutokuwa maamuzi ya kuchagua mume ampendae.

Katika wimbo wa mwana mwema mwandishi ameonesha ishara ya neno “chenga na chelele” maneno yote mawili haya yameonesha dhamira ya kupinga ubaguzi katika malezi. Hivyo basi, ishara zote kwa pamoja wasanii wamezitumia ili kuweza kuepuka uhasama na ugomvi kama maneno haya yangetumika wazi wazi.

Katika muhimili mwengine wa nadharia ya Semiotiki ni muktadha unaotumika, katika nyimbo bembelezi za watoto maneno yanayotumika yanakwenda sambamba na mazingira ya jamii inayoimbia nyimbo hizo, mfano katika wimbo wa “Kijaluba” yametumika maneno kama “Bungi pwani, kijaluba na karafuu” ambavyo vitu vyote kwa pamoja vinapatikana katika nchi ya Zanzibar, na Bungi pwani ni eneo linalopatikana katika Mkoa wa Kusini Unguja katika Wilaya ya kati. Hivyo wasanii wameyatumia maneno kwa mujibu wa muktadha wake.

4.2.3 Takriri

Kahigi na Mulokozi (1979) wanaelezea takriri kuwa ni uradidi yaani urudiaji wa sauti, silabi, neno, au sentensi katika kazi za kifasihi ili kuleta athari na maana maalumu kwa msikilizaji au msomaji wa shairi. Jilala (2016) anasema ni mtindo wa usemi ambao msemaji hurudia neno au maneno yale yale kwa lengo la kutilia mkazo au kusisitiza jambo. Wasanii wa nyimbo teule nao pia hawakuwa nyuma katika kutumia mbinu hii ya kisanaa wametumia takriri irabu, takriri silabi na takriri neno katika kutilia mkazo, mfano wa takriri hizo ni kama zilivyojitokeza katika nyimbo zifuatazo takriri irabu. Katika wimbo wa Dume kongwe imejitokeza takriri irabu (e) kwa kila ubeti mfano neno “kongwe, matonge na gombe,” takriri zote hizi zimejidhihirisha katika vina vya mwisho katika kila ubeti. Vile vile katika wimbo huo huo tunapata takriri ya silabi (nde) ambayo imejitokeza katika vina vya kati. Na pia tunapata silabi ya (ka) katika wimbo wa Msikiti wa jibondo ambayo imejitokeza katika vina vya mwisho vya kila ubeti mfano neno “zawaka, nyaraka na paka”.

Katika nyimbo bembelezi hatupati takriri irabu na silabi tu bali hata takriri maneno zimejitokeza mfano wa takriri hizo zinapatikana katika wimbo wa Usilie usilie neno “usilie na machozi” zikiwa zinatilia mkazo katika mapenzi, mahaba na imani ya dini.

4.2.4 Usimulizi

Wamitila (2008) anasema usimulizi unaopatikana katika kazi za kifasihi unaweza kuhusishwa na nafsi inayosimulia ambayo haijibainishi wazi wazi kama mhusika katika kazi inayohusika. Anaendelea kusema kuwa hali hii inatokea sana katika usimulizi wa nafsi ya pili au ya tatu ambapo anayesimulia hatambulishwi kwa njia iliyo wazi ingawa mara nyingi pana muelekeo wa kimakosa wa kuhusishwa nafsi inayosimulia na mwandishi wa kazi inayohusika. Anamalizia kwa kusema usimulizi unaweza kufanywa na mhusika au wahusika wanaopatikana katika kazi fulani ya fasihi. Hivyo basi, nyimbo bembelezi zimetumia nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu.

4.2.4.1Usimulizi wa Nafsi ya Kwanza

Mlacha (1991) anaeleza kwamba katika mbinu hii ya usimulizi mwandishi hupotelea ndani ya mmoja ya wahusika wake ambae husimulia hadithi yote. Katika mbinu hii ya usimulizi, mwandishi au msanii anasimulia matukio lakini anajikita katika muhusika mmoja tu.

Wasanii wa nyimbo bembelezi nao wameonesha matumizi ya nafsi ya kwanza katika wimbo wa Mama

Mama aliponivyaa halinyona mbaya

Kanka chakula chema na nguo njema kuvwaa

Kasoro kitu kimoja kanyiti mwana hizaya

Katika dondoo hilo lililodondolewa linaonesha usimulizi wa nafsi ya kwanza. Msimulizi katika wimbo huu ni msimulizi mhusika kwani anasimulia tukio lake lililotokea kwa mzazi wake, kuwa alipozaliwa mama wa mtoto huyo hakumuona

mbaya kwani alimpa mahitaji yote ambayo mzazi anahitajia kumpa mtoto wake. Lakini mtoto huyu anaonesha masikitiko yake ya kwamba amezaliwa nje ya ndoa, juu ya kwamba mzazi wake ana mapenzi na mahaba kwa mtoto wake.

Miongoni mwa msingi na mhimili wa nadharia ya Semiotiki ni lugha, wasanii wa nyimbo za kubembelezea watoto wamekuwa ni mahiri sana katika utumizi wa lugha na hutumia lugha fiche ambayo hupunguza makali ya matusi na maneno yasiyohitajika kusemwa hadharani, mfano katika nyimbo ya mama wasanii wametumia maneno kama mwana hizaya likiwa na maana ya mtoto wa haramu. Katika misingi wasanii wameweza kutumia lugha inavyopaswa na kustahiki ili kuepusha ugomvi na mifarakano katika jamii.

4.2.4.2 Usimulizi wa Nafsi ya Pili

Katika nyimbo bembelezi wasanii wanatuonesha nafsi ya pili katika nyimbo hizo, mfano wa wimbo huo ni Usilie usilie Kama unavyosema:

Usilie usilie ukaniliza na mie

Machozi yako yatue nikifwaa unililie

Ujibwage bwage na chii watu wakushikilie

Wenye machozi karibu nao wakusaidie

Anlelee mwanangu anlelee

Katika dondoo hiyo umetumiwa usimulizi wa nafsi ya pili katika kutilia mkazo kwa lile jambo linaloelezwa. Mzee anamzuia mwanawe asiwe na majonzi na masikitiko katika uhai wake bali adhihirishe mapenzi kwa mzazi wake, mzee anamhimiza mtoto awe miongoni mwa watoto wema aweze kumsaidia baada ya kufa kwake.

4.2.4.3 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu

Usimulizi wa nafsi ya tatu umejitokeza katika nyimbo nyingi sana za bembelezi miongoni mwa nyimbo hizo ni wimbo wa Dume Kongwe usemao:

Baba na mama wetende kunioza dume kongweee,

Halisafiri halyende kazi kupiga matongeee,

Likikaa mvunguni hunguruma kama gombeee.

Katika dondoo lililodondolewa hapo juu msanii anaonesha masikitiko kwa wazazi wake kwa kutopea nafasi ya kuwa na maamuzi ya kuchagua mpenzi ampendae. Uamuzi uliofanywa na wazazi wa kumuozesha mtoto wao mume asieridhika nae, ni sababu moja wapo ya kuonesha hudhuni zake za kutotekelezewa mahitaji ya nyumba. Na mwisho anamfananisha na gombe kwa kutoona faida yoyote kutoka kwa mume huyo.

4.2.5 Taswira

Senkoro (2011) anasema taswira ni lugha inayochora picha ya vitu au mahali kwa kutumia ishara, ni mkusanyiko wa picha mbalimbali ziundwazo na maelezo ya wasanii katika kazi ya fasihi. Senkoro (1988) anaeleza kuwa matumizi mazuri ya taswira hutegemea ufundi wa msanii au mshairi wa kuweza kuchota mambo mbalimbali yaliyomzunguka na jamii yake na pia kutoka katika historia na sehemu nyengine za maisha azijuazo. Senkoro (ameshatajwa) amezigawa taswira katika makundi matatu; taswira zinazoonekana, taswira za mawazo na taswira za hisi. Jilala (2016) anasema mbinu ya kitaswira hurejelea matumizi ya lugha yanayopambanuliwa na uteuzi mzuri wa maneno, ulinganifu na udhahiri wa maelezo yenye kuhusisha na kujumuisha dhana tofauti ili kuleta taswira na athari maalum katika mawazo ya msomaji. Wasanii wanapotumia taswira huwasilisha maudhui ya kazi zao, mfano tunapata taswira ifuatayo: katika riwaya ya Kiu (2009) mwandishi

anasema "… kila alipofika asubuhi, alimkuta Mwinyi amedhoofu kuliko alivyomuacha jana, kwa kumlilia Bahati… kila uchao, alikuwa kitandani akigalagala, mara anasema hapa panamuuma, mara pale panamuasha. Wakati wote alikuwa akimwita Bahati kwa jina, akimlilia, akisononeka, akiitazama picha yake, akiibusu na kuikumbatia" katika taswira hii msanii anaonesha dhamira ya mapenzi aliyonayo Mwinyi kwa Bahati. Hivyo basi, mbinu ya taswira imejitokeza kwa kiasi kikubwa katika nyimbo bembelezi za watoto mfano katika wimbo wa Kidau, Kijaluba na Dume kongwe nyimbo zote hizi kwa pamoja zimeonesha matumizi mbalimbali ya taswira mfano katika wimbo wa kijaluba wasanii wanasema:

Nilikwenda matembezi upande wa Bungi pwani,

Nikakuta kijaluba kina karafuu kati,

Kijaluba hali hii mwenyewe yu hali gani?

Katika wimbo huu wasanii wameonesha matumizi ya taswira ya kijaluba na karafuu. Taswira ambayo inatoa picha ya nchi na uchumi wake unaopatikana. Nchi inayoelezewa katika wimbo huu imejaa rasilimali ambayo inawapelekea wananchi wake kufaidika nayo.

4.2.6 Nahau

Ni msemo uliojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida lakini ambao huwa umesitiri maana tofauti na ile inayobebwa na maneno hayo hayo katika matumizi ya kawaida. Nahau hutumiwa kuwa ni njia ya kupanga kazi ya fasihi na pia katika kuainisha wahusika na lugha zao Senkoro (2011). Wamitila (2008) anasema zipo nahau mbalimbali zinazoweza kuwa na ufunge wa kimuuondo ambazo huonesha unyumbufu fulani wa kimaana. Wamitila anaendelea kusema kuwa unyumbufu huu

wa nahau unaonekana pale ambapo neno fulani linavyoweza kubadilishwa lakini maana yake ikabaki vile vile.

Katika nyimbo bembelezi wasanii wa nyimbo hizi nao wametumia nahau katika kuonesha dhamira walizokusudia mfano katika wimbo wa Dume Kongwe imetumika nahau kama “kupiga matonge” ikiwa na maana kuwa hakuna manufaa yoyote yanayopatikana kwa mtu huyu bali ni hasara. Katika wimbo wa Mama msanii ametumia nahau ya “mwana hizaya” ikiwa na maana ya mwanaharamu.

4.2.7 Tashbiha

Msokile (1992) anasema tashbiha ni mbinu ya kisanaa ambayo inatumia viunganishi kwa vitu viwili au zaidi vyenye hulka tofauti, tashbiha; hutumia ulinganishi wa mambo au vitu, kwa kutumia viunganishi kama vile: ja, mithili ya, mfano wa, sawa na, na kama. Mulokozi na Kahigi (1979) wanasema kuwa hii ni tamathali ya ufananisho au mlingano wa vitu viwili au zaidi. Katika tashbiha hakuna maana dhahnia, bali kuna ulinganishaji wa vitu viwili vilivyo bayana. Wasanii katika nyimbo bembelezi wameionesha mbinu hiyo, mfano wa tashbiha umebainishwa katika wimbo wa Dume Kongwe pale wasanii waliposema katika mstari wa tatu wa wimbo huo, “Likikaa mvunguni hunguruma kama gombe”. Katika mfano wa tashbiha hii wasanii wamefananisha mwanamme ambae hana uwezo wa kuyakimu maisha ya kindoa kwa kumfananisha na gombe aliyekuwa mzee ambae hana faida yoyote kwa bwana wake.

4.2.8 Usambamba

Kahigi na Mulokozi (1979) wanasema usambamba ni takriri ya sentensi au vifungu vya maneno vyenye kufanana kimaana au kimuundo. Wanaendelea kusema kuwa usambamba huonekana sana katika ushairi simulizi wanasema kuwa Shaaban Robert

ni msanii ambae amekitumia kipengele hiki mara kwa mara katika mashairi yake wametolea mfano katika shairi la kinyume kwa kusema:

Amina umejitenga kufa umetangulia,

Kama uwa umefunga baada ya kuchanua,

Nnakuombea mungu peponi kukubaliwa,

Mapenzi tuliyofunga hapana wa kuyafungua.

(Shaaban Robert katika Maisha Yangu na Baada Ya Miaka Hamsini)

Jilala (2016) anasema usambamba ni hali ya kujitokeza kwa vipengele vya lugha kwa namna ya kufanana. Anaendelea kusema kuwa usambamba ni nia mojawapo ya kuleta ushikamano wa matini katika kazi za fasihi. Nyimbo bembelezi nazo pia zimetumia mbinu hii, zimetumia usambamba katika kuibua dhamira mfano wa usambamba tunauona katika wimbo wa Mwana mwema msanii anasema: “

Ukilea mwana mwema na mwana mui mleee,

Mwema ukimka chenga na mui mke chelele,

Humwiji akufae akukae maji mbele,

Katika wimbo huu mtafiti ameona kuwa usambamba uliojitokeza unajenga mshikamano katika kuibua dhamira, dhamira ambayo wasanii wameikusudia kwa jamii, maneno kama “mwema, mui, chenga na chelele” yote kwa pamoja yanajenga dhamira ya kuepuka ubaguzi, dhamira ambayo wasanii wanataka kuiwasilisha kwa hadhira yao.

Katika wimbo wa Kidau usambamba unaonekana katika mstari usemao; siuvai, siutupi wala simki mwenzangu” wasanii wameonesha usambamba kwa kuibua dhamira ya mapenzi ya mwanamme wa nje ya ndoa anaependwa na mwanamke alie ndani ya ndoa ya mume mwengine, kwa kuonesha umuhimu wa mwanamme wa nje

ya ndoa mwanamke anaona hawezi kuolewa na wanaume wawili na wala hataki mwanamme huyo achukuliwe na mwanamke mwengine.

Kimsingi, matumizi ya mbinu za kisanaa yapo mengi sana na hayawezi kutafitiwa katika utafiti kama huu na kumalizika. Hivyo basi, katika utafiti huu mtafiti ameteuwa mbinu chache tu ili kuweza kukamilisha lengo la utafiti huu.

4.3 Hitimisho

Sura hii mtafiti amewasilisha, kuchambua na kujadili data na matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu kulingana na malengo mahsusi ya utafiti kama yalivyoainishwa katika sura ya kwanza. Sura hii imebainisha dhamira ambazo zinapatikana katika nyimbo bembelezi za watoto, pamoja na kubainisha vipengele vya mbinu za kisanaa zinazotumiwa na wasanii katika nyimbo bembelezi zilizochunguzwa.

Utafiti huu umebaini kuwa nyimbo bembelezi zilizochambuliwa zimejaa utajiri wa dhamira mbalimbali za kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi. Baadhi ya dhamira zilizojitokeza katika nyimbo hizo ni; mapenzi, malezi, nafasi ya mwanamke, elimu, uchumi, utamaduni, na siasa. Vile vile katika utafiti huu vimebainishwa vipengele mbali mbali vya mbinu za kisanaa ambavyo vimetumika katika utafiti huu, vipengele vilivyojitokeza ni pamoja na sitiari, ishara, nahau, taswira, tashbiha, takriri, masimulizi na usambamba, vipengele vyote kwa pamoja vimesaidia kuibua dhamira. Sura inayofuata inahusu

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Hii ni sura ya mwisho ambayo inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Sura hii imegawika katika sehemu kuu tatu, ambazo ni; Sehemu ya kwanza inahusu muhtasari, sehemu ya pili inahusu hitimisho na sehemu ya tatu ni mapendekezo ya utafiti huu.

5.1 Muhtasari

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza na kubainisha dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi. Utafiti ulilenga kubainisha nyimbo za watoto zinazoimbwa katika eneo la Makunduchi ambapo nyimbo nane zilishughulikiwa. Pamoja na ubainishaji wa nyimbo hizo, zilichunguzwa na kuchambuliwa dhamira mbalimbali za nyimbo bembelezi za watoto kutoka kimakunduchi. Kisha utafiti ulijielekeza katika kubainisha mbinu za kisanaa zinazotumiwa na wasanii katika kusawiri dhamira zinazopatikana katika nyimbo za watoto zilizoshughulikiwa.

Utafiti huu una jumla ya sura kuu tano. Sura ya kwanza imetoa mwelekeo wa utafiti huu kwa kubainisha vipengele kadhaa vya utafiti ukijumuisha vipengele vya utangulizi, ambacho ni kipengele muhimu kilichotowa ufafanuzi juu ya mada lengwa, usuli wa mada ulioonyesha sababu zilizopelekea utafiti huu kufanyika, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti lilibainishwa ambalo ni kuchunguza dhamira za nyimbo bembelezi za watoto, malengo mahsusi ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na kipengele cha mwisho ni mpangilio wa tasnifu. Vipengele hivi kwa hakika

ndivyo vinavyomwelekeza msomaji kwamba tasnifu hii inahusu mambo gani na kwa nini utafiti huu ulifanyika.

Sura ya pili imefafanua mapitio mbalimbali ya maandiko ya wataalamu yanayohusiana na utafiti huu. Ambapo pia ilitoa ufafanuzi wa istilahi za msingi iliyotumika katika utafiti huu, istilahi hiyo ni dhana ya bembelezi na dhamira, maelezo ya dhana hizo yalisaidia kuibua matokeo yaliyotarajiwa katika utafiti huu. Miongoni mwa mapitio yaliopitiwa ni pamoja na makala kadhaa, maandiko yaliyopitiwa yamegawanywa katika sehemu tatu, kwanza ni maandiko yaliyohusiana na nyimbo kwa jumla, pili ni maandiko yaliyohusu dhamira za nyimbo kwa jumla, tatu ni maandiko yanayohusu nyimbo bembelezi. Mwishowe mapitio yaliyodurusiwa yaliibuwa pengo la utafiti kuhusiana na mada ya utafiti huu. Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na nadharia ya Semiotiki ndizo zilizosaidia katika uchambuzi wa data wa nyimbo hizo zilizochunguzwa.

Sura ya tatu imebainisha mbinu na zana za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Sura hii imejumuisha vipengele vya utangulizi, eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, walengwa wa utafiti, sampuli na usampulishaji. Vipengele vingine ni aina za data ziliyokusanywa, data za msingi na data za upili, mbinu za kukusanyia data ambazo ni mbinu ya maktaba, ushuhudiaji, kusikiliza na mahojiano, pia zimeelezwa zana za kukusanyia data, na mchakato wa mbinu za kuchambua data, maadili ya utafiti na hatimaye ni hitimisho kwa sura hiyo.

Sura ya nne imejadili na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Sura hii imegawanywa katika sehemu mbili kulingana na malengo na masuali yaliyouongoza utafiti huu. Sehemu ya kwanza imechambua dhamira za nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi, miongoni mwa nyimbo zilizobainishwa ni kama vile; dume

kongwe, mwana mwema, msikiti wa jibondo, mama, kidau, kijaluba, mtoto wangu na usilie usilie na dhamira zilizobainishwa ni; mapenzi, utamaduni, elimu, ukweli, malezi, siasa, uchumi, nafasi ya mwanamke na sehemu ya pili imebainisha mbinu mbalimbali za kisanaa zinazotumiwa na wasanii katika nyimbo teule.

Sura ya tano ambayo imetoa muhtasari wa utafiti, hitimisho na mapendekezo ya utafiti wa baadae. Mapendekezo hayo bila ya shaka iwapo yatazingatiwa vyema yatasaidia katika kuibua hisia mpya juu ya umuhimu wa utafiti huu na tafiti nyenginezo. Msomaji anaweza kupata maudhui ya utafiti huu kwa kifupi asomapo sura hii ya tano na kuelewa utafiti mzima unahusu nini na nini unazungumzia.

5.2 Hitimisho

Katika utafiti huu lengo kuu lilikuwa ni kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi, Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi mawili ambayo yalijibiwa sambamba na maswali mawili. Malengo hayo ni; lengo la kwanza lililenga kuchambua dhamira zinazopatikana katika nyimbo bembelezi za watoto na lengo mahsusi la pili ni kubainisha mbinu za kisanaa zilizotumiwa na wasanii katika kusawiri dhamira zilizopatikana katika nyimbo teule.

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, nyimbo bembelezi za watoto mifano kutoka Makunduchi zina hadhina kubwa katika malezi na vile vile zimeweza kuibua dhamira mbalimbali zinazopatikana katika jamii ya leo. Kwa mfano dhamira kama; nafasi ya mwanamke imeoneshwa kwa mapana katika utafiti huu na matokeo yanaonesha kuwa wanawake wapewe haki sawa na wanaume hususani wakati wa kuchagua wachumba, kwani kuchaguliwa wachumba kwa upande wa wanawake kuna waletea athari kubwa katika mustakbali wao wa maisha kwa ujumla. Pia katika matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa uwepukwe ubaguzi katika malezi, watoto

wote wana haki sawa na kila mmoja anastahiki kupewa matunzo na huduma zote muhimu ambazo watoto wanahitajia. Matokeo ya utafiti kwa upande wa watafitiwa, wamethibitisha umuhimu wa kuwepo na kuendelezwa kwa nyimbo bembelezi za watoto, kwa sababu nyimbo hizo zina nafasi kubwa na nzito kwa jamii, nafasi ambazo hulenga kufikisha dhamira ziliomo ndani ya nyimbo hizo katika nyanja tofauti za kimaisha, kiuchumi, kisiasa, kijamii, kiutamaduni na hata kimaendeleo. Na nyimbo hizo zina mchango mkubwa kwa watoto katika makuzi yao na pia kwa jamii husika kwani ndani ya nyimbo hizo kunajitokeza ufikishaji wa ujumbe katika malezi kwa kupitia nyimbo bembelezi.

Kimsingi, wasanii wa nyimbo bembelezi za watoto hutumia mbinu za kisanaa katika kusawiri dhamira za nyimbo bembelezi zilizomo ndani ya nyimbo hizo, lengo mahsusi la pili limejibiwa kwani zimebainika mbinu mbalimbali ambazo zimejitokeza katika nyimbo hizo, miongoni mwa mbinu hizo ni kama ishara, sitiari, taswira, nahau, tashbiha, takriri, usambamba na usimulizi, mbinu zote kwa pamoja zimesaidia kuibua dhamira zilizojitokeza katika nyimbo hizo. Hata hivyo, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba matumizi ya mbinu ya sitiari na mbinu ya ishara ndizo zilizojitokeza mara nyingi zaidi katika nyimbo bembelezi za watoto ukilinganisha na mbinu nyengine, hali hii inadhihirisha kwamba wasanii wanatumia lugha fiche katika kuwasilisha dhamira kwa jamii husika.

Katika muktadha wa bembelezi zinaonekana kuwa zina matumizi ya ziada mbali na kubembeleza mtoto, hili linajidhirisha kutokana na hadhira lengwa ya bembelezi. Bembelezi huimbiwa watoto lakini huwahusu watu wazima na maneno haya yamethibitishwa na watafitiwa wa nyimbo hizi.

Kwa mujibu wa data zilizokusanywa kutoka uwandani, nyimbo hizi hivi sasa kwa kiasi kikubwa huimbwa na wanawake wenye umri kuanzia miaka hamsini na kuendelea. Wenye umri chini ya hapo wameshaanza kuacha kubembeleza watoto wao kwa nyimbo hizi. Na hata baadhi ya hao wanaoziimba hawazijui maana zake zilizokusudiwa wao huimba tu kubembelezea na kwa kurahisisha kazi zao za nyumbani, kama walivyoeleza hayo Ndungo na Wafula (1993) pale waliposema nyimbo hizi ziliimbwa kwa sauti nzuri na makabila mbalimbali ili kuwafanya watoto walale.

5.3 Mapendekezo

Matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa ipo haja ya kufanya tafiti nyengine katika uwanja huu wa bembelezi ili kuangalia vipengele vyengine vya fani na maudhui. Kwani bado zinahitajika tafiti za kina kuhusu matumizi ya picha, falsafa katika bembelezi, ubora na udhaifu wake kwa kuangalia zaidi mafanikio yanayopatikana.

Utafiti huu unapendekeza tafiti nyengine zifanyike kwa kutumia mifano ya sehemu mbalimbali ambazo zinapatikana Zanzibar na Tanzania kwa jumla, hususan katika maeneo ambayo sayansi na teknolojia ya utandawazi hayajaenea. Hii inasababishwa na ukweli kuwa maendeleo ya sayansi na teknolojia kama vile matumizi ya mtandao wa intaneti na vingamuzi ni vitu vinavyoathiri sana utamaduni katika maeneo ya mjini. Kwa hakika, hata mitandao ya simu bado baadhi ya sehemu ni ya taabu na hii inasababisha vijiji hivi kuwa nyuma katika nyanja hizi za mawasiliano kwa ujumla.

Mtafiti anapendekeza kufanywa kwa tafiti zaidi kwenye tanzu mbalimbali za fasihi simulizi, tafiti hizo zitazidi kuchimbuwa hazina ya maarifa yaliyofumbatwa kwenye fasihi hii. Maeneo yanayopendekezwa kufanyiwa utafiti ni kuhusu maana ya dhana muhimu na istilahi zinazotumiwa katika lugha ya nyimbo za watoto na vipera

vingine vya fasihi simulizi, sababu zinazosababisha kupotea kwa nyimbo hizo kwa jamii ya sasa na jamii inayokuja. Mapendekezo ya utafiti huu yanatarajiwa kupunguza au kuondoa kabisa mapungufu yaliyopo. Aidha utekelezaji wake utasukuma maendeleo ya fasihi simulizi kwa ujumla na kuinua hadhi ya fasihi simulizi kwa jamii. Vile vile utafiti huu utatoa mchango mkubwa kwenye taaluma ya fasihi simulizi kwa kuiongezea haiba na hadhi yake stahiki.

MAREJELEO

Adam, O. A. (2014), "Kuchunguza Dhamira za Kijamii na Kiutamaduni katika riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka *Kuli* na *Vuta N'kuvute*." Digirii ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Ali, S.A. (2013), "Athari Za Mtindo Katika Kuibua Maudhui: Mifano kutoka Bembelezi za Pemba." Tasnifu ya M.A (Kiswahili) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ali, H. (1969), *Lugha Yetu*, juz 1 na 1 uk 20 na juz 2 na 1 uk 15.

Ameir, I. H. (1983), *Misingi ya Nadharia ya Uhakiki*. Dar es Salaam: TUKI.

Andanenga, A. A. S. (2002), Bahari ya Elimu ya Ushairi. Ndanda Peramiho. Benedictine Publication.

BAKIZA (2010), *Kamusi ya Kiswahili Fasaha*, Oxford University Press: East African Limited, Kenya.

Balisidya, M. (1987), "Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi", *Mulika*, tol.19.

Bogdan, R. na Biklen, S. K. (1992), *Qualitative Research of Education: An Intropduction to Theory and Methods* (Edrs), Boston: Allyn and Bacon.

Bryman, A. (2004), *Social Research Methods* (2nd edition). Oxford: Oxford University Press.

Buliba, A na wenzake (1996), *Misingi ya nadharia na mbinu za Utafiti*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Creswell, J.W. (2009), *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publication.

Cohen, L na wenzake (2000). *Research Methods in Education 5 edition*. London: Rutledge Falmer.

Enon, J. C. (1998), *Educational Research Statistics and Measurements*, Kampala: Makerere University.

Farsy, S. A. (1956), *Ada za Harusi katika Unguja.* Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Farsy, M. S. (1967), *Ada za Harusi katika Unguja,* Kenya Literature Bureau: Nairobi.

Finnegan, R. (1970), *Oral Literature in Africa*, Nairobi: Oxford University Press.

Finnegan, R. (1979), *Oral Literature in Africa*, Great Britain: Oxford University Press.

Finnegan, R. (1994), *Oral Literature in Africa*, Dar es Salaam: Oxford University Press.

Gibbe, A. (1990), "Ufumbaji katika Ushairi wa Kiswahili," Jarida la *Kiswahili,* toleo namba.1na.2. Dar es Salaam: TUKI, kur 12-28.

Gora, H. G. (2011), "Mitindo ya Nyimbo za Uganga wa Pepo," Chuo Kkuu cha Dodoma. Tanzania.

Haji na wenzake (1992), *Uhakiki wa Fasihi Kidato cha Kwanza*. Zanzibar: E.W.W. Mbweni.

Haji, A.I. (1992), *Fasihi, Katika Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*, Zanzibar: TAKILUKI.

Haji, O. M. (2006), *Vipera vya Fasihi Simulizi*, Dar es Salaam: Tanzania Central Printing Services.

Hamad, A. (2008), *Matumizi ya ushairi na Muziki wa Kiswahili katika maisha ya kila siku Pwani ya Afrika ya mashariki.* Zanzibar: Bakiza.

Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi, Nadharia, Mbinu na Matumizi*. Dar es Salaam: Daudi Publishing Company.

Kahigi, K. K. (1995), *Lugha katika Vitabu vya Watoto,'' katika Kioo cha Lugha*. Na.1. TUKI: Dar es Salaam. Kur 15-26.

Kapury, (1993), *Oral Literature of the Masai*, Nairobi: East Africa Education Publishers.

Karisa, B. S. (2000), *Kitangulizi cha Mbinu za Uchambuzi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Oxford University Press.

Kezilahabi, E. (1988), *Rosa Mistika,* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

King'ei, K. na Kisovi, C. N. M. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi,* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing*: *Introduction,* Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, R. C. (2004). *Research Methodology*: *Methods and Techniques*, New Delhi: New age International (P) Limited Publishers.

Kothari, R. C (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*, New Delh: New age International Publishing Ltd.

Kothari, R.C. (2013). *Research Methodology: Methods and Techniques,* 2nd Ed, New Age International (P) Ltd: New Delhi.

Kumar (1999), Research Methodology: A Step- by- Guide for Beginners. New Delhi: S AGE Publication.

Masebo, J. A na Nyangwine, N (2004), *Nadharia ya Fasihi, Kiswahili 2*, Dar-es-Salaam, Afroplus Industries Ltd.

Matter, L. (1989), *Tanzu za Fasihi Simulizi, Mulika na 19*, Dar es Salaam, Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili.

Mbarouk, A. A. (1983), *Nyimbo za Michezo ya Watoto: Katika Fasihi Simulizi*, Zanzibar TAKILUKI, Dar es Salaam: T.P.H.

Mbarouk, S.S. (2011), *Athari za Semi za Kanga Katika Jamii*, Tasnifu kwa Ajili ya Shahada ya Pili, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mbogo, E. (2002), *Watoto wa Mama Ntilie*, Dar es salaam: HEKO. Publishers.

Mhilu, G na Wenzake (2008), *Tahakiki Vitabu teule vya Fasihi Kidato cha 3 na 4 Nadharia Uhakiki na Maswali*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Mlama, P. (1972), *Hatia*, Nairobi: East African Publishing House.

Mlacha, S. A. K. na Hurskeinein, A. (1996), *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*, TUKI: Dar es Salaam.

Mngaruthi, T.K. (2008), *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Founation.

Mohamed, M.S (1972). *Kiu*, Nairobi: Longman.

Mohamed, S. A. (2011). *Tata Za Asumini*, Dar es Salaam: Longman Publishers.

Msokile, M. (1981), "Nafasi ya nyimbo za Fasihi simulizi katika jamii iliyoandikwa," *Makala za Fasihi Simulizi*, Dar es Salaam: DUP.

Msokile, M. (1992), *Kunga za Fasihi na Lugha,* Dar es Salaam: Educational Publisher and Distributers L.T.D.

Mulokozi, M. M. (2003), "Tanzu na vipera vya Fasihi Simulizi," *Makala za Semina ya*

Kimataifa ya Waandishi wa Fasihi, Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. (1989), "Tanzu za fasihi simulizi," *Mulika* na 21 uk 1-21

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*, Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M na Kahigi, K. K. (1979), *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mutembei, K. A. (2012), *Korasi katika Kiswahili*: *Nadharia mpya ya Uhakiki*, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Mvungi, T. (1995), *Mashairi ya Chekacheka*, Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors.

Mzee, J. (2011). "Athari za Nyimbo za Mipasho kwa Jamii ya Wazanzibar," Tasinifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Dodoma.

Ndugo, M na Wafula, N. (1993), *Tanzu za fasihi simulizi*, Nairobi: University of Nairobi.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999), *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta: Foundation Nairobi, Kenya.

Nkwera, F. V. M. (1978), *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo*, Dar-es-salaam: DUP.

Nyangwine, N na Wenzake (2004) *Tahakiki ya Vitabu Teule vya Fasihi Kidato cha 3 na 4 (2004-2007) Ushairi, Riwaya, Tamthilia*. Afroplus Industries Ltd. Dar es salaam. Tanzania.

Omary, M. (2011), "Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008), Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Omary, M. (2015), "Kuchunguza Ufasihi Simulizi katika Kazi za Euphrase Kezilahabi Mifano ya vitabu vya *Kichomi* (1974), *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008)," Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Othman, S.Y. (2007), *Lullabies: Women Wring Africa*. Nairobi: The Eastern Region Feminist Association.

Robert, S. (2003). *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*, Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Rwezaura, T. (1981), *Sheria za ndoa Tanzania*, Dar es Salaam: TUKI.

Sengo, T. Y (1995), *Itikadi katika jamii za Kiswahili, Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*, Dar es Salaam: EALB.

Sengo, T. S.Y.M. (2009), *Sengo na Fasihi za Kinchi*, Dar es salaam: AERA.

Sengo, T. S.Y. M. na Kiango, S. (2012). Hisiya zetu, Dar-es-salaam: TUKI.

Sengo, T .S.Y.M (2014), *Falsafa ya Maisha*, Dar es Salaam: Hakijachapishwa.

Senkoro, F. E. M. K. (1987), *Fasihi na Jamii*, Dar es salaam: Press and Publicity center.

Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia na tahakiki*. Dar es Salaam: DUP.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*, Dar-es-salaam: Kauttu Limited.

Shafi, A. S (1979), *Kuli*, Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Shafi .A. S. (1999), *Vuta N'kuvute,* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Taassisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar (1983), *Fasihi simulizi*, Zanzibar: Tanzania Publishers House.

Taasisi ya Elimu na Ukuzaji Mitaala (1988), *Kiswahili Sekondari*. Zanzibar: Taasisi ya Ukuzaji Mitaala.

TUKI, (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*: Oxford University Press.

TUKI, (2013), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (toleo la 3) Nairobi: Oxford University Press.

Walliman, N. (2011) *Research Methods: The Bases*, Routledge, London and New York.

Ussi, H.M. (2009), "Dhima ya Michezo ya Watoto ya Jadi katika Jamii ya Wamakunduchi Zanzibar," Tasnifu ya Uzamili I.U.I.U (haijachapishwa).

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Sai industrial Ltd.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi: Phonex Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya fasihi istilahi na nadharia*, Focus Publications Ltd.

Wamitila, K. W. (2007). *Kichocheo cha Fasihi*, Nairobi: English Press.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya fasihi 1: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*, Nairobi: Vide ~ Muwa Publishers Ltd.

Young, P. V. (1984). *Scientific Social Survey and Research*, Enalewood Cliffs: Prentice Hall of India.

htpp/www.ackyshine. com. Imepakuliwa 23/9/2016 saa 04: 48 asubuhi.

Www. Gaf. kosoft. Com/swa/nyimbo. Imepakuliwa 25/8/2016 saa 02:16 usiku.

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho 1

Muongozo wa usaili kwa wazee na watumiaji wa nyimbo za kubembelezea watoto

Utangulizi

Mimi ni mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika Kiswahili ninayesoma katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti huu kama sehemu ya masharti ya kukamilisha utafiti wangu. Hivyo basi ninaomba ushirikiano wako ili niweze kutimiza adhma hii muhimu katika taaluma ya Kiswahili.

Maswali

1) Naomba jina lako kwa ukamilifu tafadhali.
2) Unafahamu nini juu ya nyimbo bembelezi za watoto.
3) Nitajie nyimbo bembelezi za watoto unazozielewa.
4) Watumiaji wakuu wa nyimbo bembelezi za watoto ni kina nani.

   Unafikiri nyimbo bembelezi za watoto zina dhamira na ujumbe gani katika jamii.
5) Jee, nyimbo bembelezi za watoto zina mchango wowote kwa jamii.

6) Unafikiri ni kwa nini nyimbo bembelezi za watoto zimeanza kupoteza uhalisia wake.
7) Jee, kuna umuhimu wowote wa kuendelea kuwepo nyimbo bembelezi za watoto.
8) Toa maoni yako kuhusiana na nyimbo bembelezi za watoto.

Ahsante kwa mashirikiano

Kiambatanisho namba 2

Muongozo wa usaili kwa wanafunzi wa vyuo vikuu

Utangulizi

Mimi ni mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika Kiswahili ninayesoma katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Nimefanya utafiti huu kama ni sehemu ya masharti ya kukamilisha utafiti wangu. Hivyo basi ninaomba ushirikiano wako ili niweze kutimiza adhma yangu katika taaluma ya Kiswahili.

1) Naomba nitajie jina lako kwa ukamilifu tafadhali.
2) Unafahamu nini juu ya nyimbo bembelezi za watoto.
3) Nitajie nyimbo za watoto unazozifahamu.
4) Eleza dhamira zinazopatikana katika nyimbo za kubembelezea watoto.
5) Lugha ni kipengele muhimu katika kukuza na kuendeleza dhamira katika kazi za fasihi. Nitajie vipengele vya lugha vinavyopendwa kutumiwa na wasanii wa nyimbo za kubembelezea watoto.
6) Unadhani ni kwa nini wanapenda kutumia vipengele hivyo.
7) Toa maoni yako kuhusiana na nyimbo hizo.

Ahsante kwa mashirikiano yako

Kiambatanisho namba 3

Nyimbo bembelezi za watoto zilizochambuliwa

1 Mtoto wangu

Ooooh mtoto ooooh mtoto,

Mtoto wangu mzuri iiii,

Chamveleka skuli iiii,

Mtoto wangu mbaya aaaa,

Chamveleka Ulaya aaa,

Ooooh mtoto oooh.

Kiswahili Sanifu

Owa mtoto owa mtoto

Mtoto wangu mzuri iii,

Nitampeleka skuli iii,

Mtoto wangu mbaya aaa,

Nitampeleka Ulaya aaa,

Ooooh mtoto ooooh.

2 Usilie Usilie

Usilie usilie ukaniliza na mie,

Machozi yako yatuwe nikifwa uninilie,

Ujibwage bwage na chii,

Watu wakushikilie,

Wenye machozi karibu nao wakusaidie,

Anlelee mwanangu anlelee.

Kiswahili Sanifu

Usilie usilie ukaniliza na mie,

Machozi yako yaweke nikifa uninilie,

Ujiangushe angushe na chini,

Watu wakushikilie,

Wenye machozi karibu na wao wakusaidie.

3 Kijaluba

Nyevu nende matembezi upande wa Bungi pwani,

Nikakuta kijaluba kina karafuu kati,

Kijaluba hali hii mwenyewe yu hali gani,

Ooooh mtoto ooooh.

Kiswahili Sanifu

Nilikwenda matembezi upande wa Bungi pwani,

Nikakuta kijaluba kina karafuu ndani,

Kijaluba hali hii mwenyewe yuko hali gani,

Ooooh mtoto ooooh.

4 Kidau

Kile kidau kijacho nnageza mna changu,

Mna mkufu nitunge kadiri ya shingo yangu,

Siuvai siutupi wala simkii mwenzangu,

Chamka mama mzazi msiri wa mambo yangu,

Bwana wewe sikwebu waninyezeza nini kwangu?

Kiswahili Sanifu

Kile kadau kijacho hamkosi mna changu,

Mna mkufu nivae kadiri ya shingo yangu,

Siuvai siutupi wala simpi mwenzangu,

Nitampa mama mzazi msiri wa mambo yangu,

Bwana wewe sikutaki wanifata nini kwangu?

5 Mwana mwema

Ukilea mwana mwema na mwana mui mleee,

Mwema ukimka chenga na mui mke chelele,

Humwiji akufae akukae maji mbele,

Kisawahili Sanifu

Ukilea mwana mwema na mwana mui mlee,

Mwema ukimpa chenga na mui mpe chelele,

Humjui akufaaye akupae maji mbele.

6 Dume Kongwe

Baba na mama wetende kunioza dume kongweee,

Halisafiri halyende kazi kupiga matongeee,

Likikaa mvunguni hunguruma kama gombeee.

Kiswahili Sanifu

Baba na mama watende kuniozesha mwanamme mkongwe,

Halisafiri haliendi kazi kupiga matongwe,

Likilala mvunguni hunguruma kama ng'ombe.

7 Mama

Mama aliponivyaa halinyona mbaya,

Kanka chakula chema na nguo njema kuvwaa,

Kasoro kitu kimoja kanyiti mwana hizaya.

Kiswahili sanifu

Mama aliponizaa hakuniona mbaya,

Kanipa chakula chema na nguo njema za kuvaa,

Kasoro kitu kimoja kanita mwana wa haramu.

8 Msikiti wa jibondo

Msikiti wa jibondo kandili mbili zawakaa,

Wamo wasomaji vyuo na waandikao nyarakaa,

Nyama zote nzili kasoro kia lya pakaa.

Kiswahili Sanifu

Msikiti wa jibondo kandili mbili zinawaka,

Wamo wasomaji vyuo na waandikao nyaraka,

Nyama zote nimekula kasoro kia la paka.